**KATIKA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU, ARUSHA**

**OMBI LA MAONI YA USHAURI NA 002 LA 2026**

# KUHUSU OMBI LA CHAMA CHA WANASHERIA WA AFRIKA (PALU) LA KUPATA MAONI YA USHAURI KUHUSU WAJIBU WA NCHI ZA AFRIKA, NCHI MOJA MOJA NA KWA PAMOJA, KUHUSIANA NA WAJIBU BINAFSI WA JINAI KWA UKIUKAJI MKUBWA, WA HALI YA JUU AU MBAYA WA HAKI ZA BINADAMU NA WATU BARANI AFRIKA

*(Limetolewa chini ya Kifungu cha 58(1)-(3) cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu; Kifungu cha 3, 4, 7 na 33 cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu; Kanuni ya 29(1)(b) na 82 ya Kanuni za Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, 2020; na vifungu vingine vyote vya kisheria vinavyowezesha)*

# YALIYOMO


Utangulizi 5

Taarifa za Waandishi 5

Taarifa kuhusu Mamlaka ya Kisheria na Ukubalifu 6

Mazingira yanayosababisha kuleta ombi hili 6

Sheria Inayotumika 12

Masuala ya Kuamua 14

Muhtasari wa Hoja 15

Maana, Maudhui na Wigo wa Ukiukaji Mkubwa, au wa Hali ya Juu wa Haki za Binadamu na Watu 15

Wajibu wa Kuchunguza na Kufungua Mashtaka 19

Utumiaji wa Wajibu wa Kuchunguza na Kufungua Mashtaka Nje ya Mipaka ya Nchi 31

Mamlaka ya Haiba Amilifu na Si amilifu 31

Wajibu wa Mamlaka ya Kimataifa 33

Wajibu Husika wa Pamoja wa Nchi za Afrika chini ya Uundaji wa Umoja wa Afrika 38

Wajibu Husika wa Pamoja wa Nchi za Afrika chini ya Uundaji wa Jumuiya Mbalimbali za Kiuchumi za Kikanda 42

Msimamo wa PALU kuhusu Maswali Yaliyoulizwa 46

Muhtasari wa Ombi 47

Hitimisho 49

## I. UTANGULIZI

1. Hili ni Ombi la Kupata Maoni ya Ushauri lililowasilishwa na Chama cha Wanasheria (hapa hurejelewa kama "PALU" au "Mleta Maombi"), ambalo ni shirika la Afrika ambalo linatambuliwa na Umoja wa Afrika kupitia Mkataba wa Makubaliano ("MoU") uliowekwa mwaka 2006 meambatishwa hapa kama (Kiambatisho cha 1 cha hati hii).

2. PALU ni chama cha bara zima cha mawakili na wataalamu wengine wa sekta ya sheria na mashirika, kilichosajiliwa na ambacho anwani yake ni 1 Barabara ya Kaunda, mkabala na Barabara ya Haile Selassie, S.L.P. 6065, Arusha, Tanzania, Simu: +255685078794, Barua pepe: legal@lawyersofafrica.org.

## II. TAARIFA ZA WAANDISHI

3. Kwa madhumuni ya Ombi hili, mawasiliano yote ya ziada yanaweza kuelekezwa kwa –


***Bw. Donald Deya, Wakili***
Chama cha Wanasheria wa Afrika (PALU),
1 Barabara ya Kaunda, Mkabala na Barabara ya Haile Selassie,
S.L.P 6065, Arusha, Tanzania.
Barua pepe: legal@lawyersofafrica.org

***Prof. Chidi Anselm ODINKALU, Wakili***
kupitia kwa Chama cha Wanasheria wa Afrika (PALU),
1 Barabara ya Kaunda, Mkabala na Barabara ya Haile Selassie,
S.L.P 6065, Arusha, Tanzania
Simu: +234 805 502 7273
Barua pepe: chidiao@hotmail.com

***Dkt. Owiso OWISO, Wakili***
OLC Law, LLP

CMS Africa House, Ghorofa ya 11
Mtaa wa Chania
S.L.P. 10191–00200 Nairobi, Kenya.
Simu: +254700033300
Barua pepe: owiso.owiso@protonmail.ch / owiso.owiso@gmail.com

***Bi. Ruth OGBEWEKON***
Chama cha Wanasheria wa Afrika (PALU),
1 Barabara ya Kaunda, Mkabala na Barabara ya Haile Selassie,
S.L.P 6065, Arusha, Tanzania.
Barua pepe: legal@lawyersofafrica.org

4. Lugha inayopendelewa na waandishi kwa madhumuni ya mawasiliano ni Kiingereza.

## III. TAARIFA KUHUSU MAMLAKA YA KISHERIA NA UKUBALIFU

5. PALU kwa heshima inaomba utekelezaji wa mamlaka ya ushauri ya mahakama hii tukufu kwa mujibu wa yafuatayo:

   a) Kifungu cha 58(1)-(3) cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu.

   b) Kifungu cha 3(1), 4(1) na 7 cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa Uanzishwaji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Itifaki ya Mahakama ya Afrika); na

   c) Kanuni ya 29(1)(b) na 82 ya Kanuni za Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, 2020 (Kanuni za Mahakama).

6. Kwa umahususi zaidi, PALU inatafuta Maoni ya Ushauri kuhusu wajibu wa Mataifa ya Afrika, taifa moja moja na kwa pamoja, kuhusiana na wajibu binafsi wa jinai kwa ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu barani Afrika.

7. Ombi hili linatoa wito kwa mamlaka ya ushauri ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) kutafsiri masharti ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba wa Afrika), hasa Kifungu cha 1 na 58 cha Mkataba.

8. Suala linalohusika katika Ombi hili halihusiani na suala linalochunguzwa na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Tume ya Afrika).

## IV. MAZINGIRA YANAYOSABABISHA KULETA OMBI HILI

9. Nchi za Afrika, kupitia Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (hapa unarejelewa kama "Mkataba"), zimejizatiti kikamilifu kulinda na kukuza haki na uhuru wa watu wa Afrika. Aya ya nane ya utangulizi inahusiaha haki na uhuru uliowekwa katika Mkataba na maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kitamaduni ya watu wa Afrika.[1]

10. Aidha, Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika (hapa inarejelewa kama "Sheria ya Kikatiba") vilevile inatambua "janga la migogoro," ambalo linaathiri maendeleo ya bara, na inasisitiza haja ya kuhamasisha amani, usalama na utulivu kama sharti la utekelezaji wa "ajenda yetu ya maendeleo," huku pia ikithibitisha dhamira ya Nchi Wanachama ya "kukuza na kulinda" haki za binadamu na watu.[2]

11. Hasa, Nchi Wanachama zilizosaini Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika zinaahidi kutetea na kulinda haki za binadamu kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu;[3] na zinatambua "haki ya Umoja kuingilia kati katika Nchi Mwanachama kwa mujibu wa uamuzi wa Baraza kuhusiana na hali mbaya, yaani: uhalifu wa kivita, mauaji ya kimbari na uhalifu dhidi ya ubinadamu."[4]

---

[1]Aya za Utangulizi, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu.
[2]Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika.
[3]Id., Kifungu cha 3(h).
[4]Id., Kifungu cha 4(h).

12. Kwa hivyo, maslahi ya maendeleo ya Afrika yanategemea uzingatiaji wa utawala wa sheria, ulinzi na utetezi wa haki za binadamu na watu na udumishaji wa amani na utulivu. Hii inaimarishwa zaidi na Ajenda ya Umoja wa Afrika ya 2063 (Afrika Tuitakayo),[5] ambayo inathibitisha ajenda ya kupambana na kutokujali sheria na inatazamia Afrika inayoongozwa kwa, na iliyojikita kwenye, utamaduni mjumui wa utawala bora, maadili ya kidemokrasia, usawa wa kijinsia, kuheshimu haki za binadamu, haki, na utawala wa sheria.

13. Licha ya kuwepo kwa makubaliano haya ya kisheria katika ngazi ya bara, Mleta Maombi anaiomba Mahakama hii Tukufu itambue kuhusu ukweli kwamba ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu na mbaya wa haki za binadamu na watu unaendelea kufanywa na wahusika wa Serikali na wasio wa Serikali katika eneo la Nchi Wanachama zilizosaini Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu. Uwajibikaji kwa ukiukaji huu kwa kiasi kikubwa umebaki kutokuwa dhahiri, kutokamilika, au kutofahamika, na kusababisha hali ya kuendelea kutoadhibiwa na kuzidisha zaidi ukosefu wa utulivu katika maeneo mengi ya bara.

14. Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu unaeleza kwamba, Tume ya Afrika inapoona kutokana na utaratibu wake wa mawasiliano kwamba mawasiliano ya mara moja au zaidi "yanaonekana kuhusiana na kesi maalumu ambazo zinaonyesha uwepo wa mfululizo wa ukiukaji mkubwa au mkubwa sana wa haki za binadamu na watu",[6] Tume inaweza kuwasilisha jambo hilo kwenye Baraza la Wakuu wa Nchi na Serikali,[7] ambalo linaweza kuomba Tume ifanye utafiti wa kina wa mambo haya "na kuandaa ripoti ya ukweli wa mambo, pamoja na matokeo na mapendekezo yake."[8]

---

[5]Ajenda ya AU 2063, Afrika Tuitakayo - https://au.int/en/agenda2063/overview
[6]Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, Kifungu cha 58(1).
[7]Id., Kifungu cha 58(2).
[8] Id.

15. Kifungu hiki cha Mkataba wa Afrika kinatambua wazi kuwepo kwa kategoria ya kanuni ya "ukiukaji mkubwa na wa kiasi kikubwa" wa haki za binadamu na watu barani Afrika. Hata hivyo, wigo na asili ya majibu yanayoruhusiwa chini ya Mkataba huu haiko dhahiri. Katika utendaji wa taasisi zilizoundwa chini ya Mkataba wa Afrika, ikiwemo Mahakama hii tukufu, hakuna mwongozo rasmi kuhusu maana au wigo wa "ukiukaji mkubwa na wa kiasi kikubwa" au kuhusu asili na wigo wa hatua ambazo zinaweza kutekelezwa ili kuyashughulikia.

16. Pengo hili lina matokeo mabaya kwenye haki za binadamu na watu barani Afrika. Mojawapo ya matukio mabaya zaidi katika historia ya hivi karibuni ya binadamu, Mauaji ya Kimbari dhidi ya Watutsi nchini Rwanda mwaka 1994, yalisababisha Shirika la Umoja wa Afrika mwaka 1998 kuunda Jopo la Kimataifa la Watu Mashuhuri (IPEP) ili kubaini ukweli kuhusu mauaji hayo ya kimbari, kupendekeza hatua za kurekebisha matokeo yake na kuzuia uwezekano wa kutokea tena. Katika ripoti yake iliyochapishwa mwaka 2000, Jopo lilipendekeza, miongoni mwa mambo mengine, ufafanuzi wa wajibu wa kisheria wa Nchi kuhusiana na uhalifu wa mauaji ya kimbari na kutafuta mamlaka ya kimataifa kama njia ya kutafuta uwajibikaji kwa mauaji ya kimbari.[9]

17. Angalau, madhara yaliyotokea nchini Rwanda mwaka 1994 na mapendekezo thabiti ya Jopo yalipaswa kuwa kama wito wa kuimarisha ulinzi wa haki barani Afrika na kuongoza kasi ya bara kuelekea kuwa na mbinu thabiti zaidi ya kuzuia ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu.[10] Hata hivyo, katika siku za hivi karibuni, bara hili limeshuhudia vurugu zaidi katika Mataifa kadhaa, zenye sifa ya ukiukaji

[9]Jopo la Kimataifa la Watu Mashuhuri, 'Rwanda: Mauaji ya Kimbari Yanayoweza Kuzuiwa' (2000), sura ya 24.

[10]Kwa umahususi, ripoti hiyo ilielezea wazi hitaji la taasisi ya kikanda yenye uwezo wa kuchukua hatua thabiti zaidi katika mazingira ya ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu na watu, ambayo ilichangia uwekaji wa sheria baadaye katika Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika kuhusu haki ya Umoja wa Afrika kuingilia kati katika Nchi Mwanachama 'kuhusiana na hali mbaya, yaani: uhalifu wa kivita, mauaji ya kimbari na uhalifu dhidi ya binadamu'.

mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu, ambazo baadhi yake zimeangaziwa hapa chini.

18. Mnamo Desemba 2007, mapigano makali yalitokea nchini Kenya kufuatia uchaguzi wa urais uliokuwa na utata, na kusababisha vifo vya takriban watu 1,300 na maelfu kujeruhiwa na kuwa wakimbizi wa ndani. Mnamo Januari 2008, Umoja wa Afrika uliitisha Jopo la Watu Mashuhuri wa Afrika likiongozwa na Katibu Mkuu wa zamani wa Umoja wa Mataifa, Kofi Annan, ambalo haraka lilifanya upatanisho na kukomesha vurugu.[11] Hata hivyo, licha ya Ripoti ya Oktoba 2008 ya Tume ya Uchunguzi wa Ghasia za Baada ya Uchaguzi (CIPEV) ambayo iliandika ukiukaji mkubwa, mbaya na wa kiwango kikubwa wa haki za binadamu unaofikia kiwango cha uhalifu dhidi ya binadamu na ambayo ilipendekeza uwajibikaji wa jinai,[12] mashtaka ya ndani hayakufanywa kamwe na kesi zote zilizofunguliwa mbele ya Mahakama ya Kimataifa ya Jinai hatimaye zilianguka katikati ya madai ya kuwapoteza mashahidi.[13]

19. Mwaka 2009, Jopo la Ngazi ya Juu la Umoja wa Afrika kuhusu Darfur lilirekodi ukiukaji mkubwa na mbaya wa haki za binadamu na watu huko Darfur, Sudan tangu angalau mwaka 2003,[14] huku ukiukaji ukiendelea hadi leo. Kuhusiana na Sudan Kusini, mwaka 2014 Tume ya Uchunguzi ya Umoja wa Afrika kuhusu Sudan Kusini iliripoti ukiukaji mkubwa, wa mara kwa mara au mbaya sana wa haki za binadamu na watu tangu Desemba 2013,[15] huku ukiukaji huo ukiendelea hata baada ya kutia saini tena

[11] Tazama Ofisi ya Jopo la Watu Mashuhuri wa Afrika ya Umoja wa Afrika, Back from the Brink; The 2008 Mediation Process and Reforms in Kenya (African Union 2014); Tinashe Sithole na Lucky E. Asuelime, 'The Role of the African Union in Post-Violence in Kenya' (2017) 6 African Journal of Governance and Development 97.
[12] Ripoti ya Tume ya Uchunguzi wa Vurugu za Baada ya Uchaguzi (CIPEV) (Oktoba 2008), sura za 3–13.
[13] Mahakama ya Kimataifa ya Jinai, 'Hali katika Jamhuri ya Kenya' https://www.icc-cpi.int/kenya.
[14] Ripoti ya Jopo la Ngazi ya Juu la Umoja wa Afrika kuhusu Darfur, PSC/AHG/2(CCVII) (Oktoba 2009), aya za 36–127.
[15] Ripoti ya Mwisho ya Tume ya Uchunguzi ya Umoja wa Afrika kuhusu Sudan Kusini (tarehe 15 Oktoba 2014) (Ripoti ya AUCISS), sura ya III, aya za 380–827 na 1122–1137.

makubaliano ya amani mwezi Septemba 2018.[16] Mwaka 2015, ujumbe wa ukusanyaji wa taarifa nchini Burundi wa Tume ya Afrika uliripoti ukiukaji mkubwa na mbaya uliofanyika tangu mwezi Aprili mwaka 2015.[17] Nchini Ethiopia ukiukaji kama huo umeripotiwa kufanywa tangu Novemba 2020.[18] Hivi karibuni, Ujumbe Huru wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa wa Kutafuta Ukweli nchini Sudan uliripoti ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu wa haki za binadamu na watu uliofanywa nchini Sudan tangu mwaka 2023.[19]

20. Matukio yaliyotajwa katika aya za 16-19 hapo juu yanawakilisha tu sehemu ndogo iliyochaguliwa ya ruwaza pana zaidi. Hasa, bara hili limekumbwa na migogoro mikubwa kama vile vurugu za baada ya uchaguzi nchini Côte d'Ivoire mwaka 2010,[20] ambayo ilitokea baada ya uchaguzi wa rais wenye

[16]Angalia Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu nchini Sudan Kusini, A/HRC/34/63 (tarehe 6 Machi 2017), aya ya 24–52; Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu nchini Sudan Kusini, A/HRC/37/71 (tarehe 13 Machi 2018), aya ya 23–110; Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu nchini Sudan Kusini, A/HRC/40/69 (tarehe 20 Februari 2019), aya ya 24–53 & 62–108; Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu nchini Sudan Kusini, A/HRC/43/56 (tarehe 20 Februari 2020), aya ya 25–75; Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu nchini Sudan Kusini, A/HRC/46/53 (tarehe 19 Februari 2021), aya ya 27–72; Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu nchini Sudan Kusini A/HRC/49/78 (tarehe 16 Machi 2022); Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu nchini Sudan Kusini A/HRC/52/26 (tarehe 31 Januari 2023), aya ya 32–94; Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu nchini Sudan Kusini, A/HRC/55/26 (tarehe 1 Machi 2024), aya ya 23–63; Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu nchini Sudan Kusini, A/HRC/58/27 (tarehe 28 Februari 2025), aya ya 19–74.

[17]Ripoti ya Ujumbe wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kazi yake ya Kutafuta Ukweli nchini Burundi, tarehe 7–13 Desemba 2015, aya za 40–167.

[18]Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu ya Ethiopia (EHRC)/Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa (OHCHR) ya Uchunguzi wa Pamoja kuhusu Madai ya Ukiukaji wa Sheria za Kimataifa za Haki za Binadamu, Sheria za Masuala ya Kibinadamu na Sheria za Wakimbizi Uliofanywa na Wahusika Wote wa Mgogoro katika Mkoa wa Tigray wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia (2021), aya za 83–354; Ripoti ya Tume ya Kimataifa ya Wataalamu wa Haki za Binadamu nchini Ethiopia, A/HRC/51/46 (tarehe 19 Septemba 2022), aya za 25–99; Ripoti ya Tume ya Kimataifa ya Wataalamu wa Haki za Binadamu nchini Ethiopia, A/HRC/54/55 (tarehe 18 Septemba 2023), aya za 20–73; Matokeo ya Uchunguzi wa Kina na Maamuzi ya Kisheria, Tume ya Kimataifa ya Wataalamu wa Haki za Binadamu nchini Ethiopia, A/HRC/54/CRP.3 (tarehe 13 Oktoba 2023), aya za 98–503.

[19]Ripoti ya Ujumbe Huru wa Kimataifa wa Kutafuta wa Ukweli nchini Sudan, A/HRC/57/23 (tarehe 5 Septemba 2024), aya za 37–95; Matokeo ya Uchunguzi Uliofanywa na Ujumbe Huru wa Kimataifa wa Kutafuta Ukweli nchini Sudan Kuhusu Ukiukaji wa Sheria ya Kimataifa ya Haki za Binadamu na Sheria ya Kimataifa ya Masuala ya Kibinadamu na Uhalifu Unaohusiana Nao, Uliofanywa nchini Sudan Katika Muktadha wa Mgogoro Ulioibuka Katikati ya Mwezi Aprili 2023, A/HRC/57/CRP.6 (tarehe 23 Oktoba 2024), aya za 124–295.

[20]Ripoti ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Hali ya haki za binadamu nchini Côte d'Ivoire, A/HRC/16/79 (tarehe 25 Februari 2011); angalia pia Côte d'Ivoire, Ripoti za Nchi za Mwaka 2010 kuhusu Mwenendo wa Haki za Binadamu, Ofisi ya Idara ya Demokrasia, Haki za Binadamu na Kazi ya Marekani (tarehe 8 Aprili 2011).

kubishaniwa na kusababisha majeruhi na raia kuhama makazi yao kwa kiwango kikubwa. Somalia, yenye miongo kadhaa ya migogoro ya muda mrefu iliyo na sifa ya kuwa na taasisi dhaifu za serikali, uwepo wa makundi yenye silaha yenye msimamo mkali na majanga ya kibinadamu yanayoendelea.[21] Jamhuri ya Afrika ya Kati pia imeathiriwa na vurugu za mara kwa mara zinazoendeshwa na kuenea kwa makundi yenye silaha, mivutano ya kijamii na miundo dhaifu ya utawala.[22] Wakati huo huo, hali katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, (hasa mashariki mwa nchi), inaendelea kuzidi kuwa mbaya, kwani wanakabiliwa na ukosefu wa usalama wa kudumu unaochochewa na makundi yenye silaha, ushindani wa rasilimali za asili na mienendo ya kuvuka mipaka.[23] Mali na Muunganp wa Nchi za Sahel (AES) pia wamekumbwa na ongezeko la ukosefu wa utulivu unaohusishwa na kutumia mamluki, uasi wenye vurugu na mazingira yanayozidi kuwa mabaya ya ulinzi wa raia.[24]

21. Eneo pana la Sahel linaendelea kukabiliana na migogoro inayohusiana inayojulikana kwa msimamo mkali wenye vurugu, mabadiliko ya tabia nchi na uwepo mdogo wa serikali. Aidha, Nigeria inaendelea kukabiliwa na changamoto sambamba za usalama, ikiwemo uasi katika eneo la kaskazini-mashariki, uhalifu wa kikatili katika eneo la kaskazini-magharibi, magenge yenye silaha katika eneo la kusini na vurugu za kikabila katika eneo la Kati.[25] Libya pia bado imegawanyika kufuatia kuanguka kwa mamlaka ya serikali kuu mwaka 2011, huku serikali pinzani na wahusika wenye silaha wakidhoofisha matumaini ya amani ya kudumu na maridhiano ya kitaifa.[26]

---

[21]Ripoti ya Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika kuhusu Hali nchini Somalia, PSC/PR/4(CCLXXII) (tarehe 21 Aprili 2011); angalia pia Wasifu wa Nchi wa Amnesty International kuhusu Somalia (2025), ilifikiwa tarehe 12 Machi 2026.
[22]Jamhuri ya Afrika ya Kati, Ripoti ya Katibu Mkuu, UNSC S/2023/769 (tarehe 16 Oktoba 2023) – ilifikiwa tarehe 11 Machi 2026.
[23]Angalia Shughuli za Silaha katika Eneo la Kongo (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo dhidi ya Uganda), Hukumu, I.C.J. Rep. 2005, 168.
[24]Shughuli za Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Afrika Magharibi na Sahel, Ripoti ya Katibu Mkuu, UNSC S/2025/77 (tarehe 28 Novemba 2025) – ilifikiwa tarehe 20 Aprili 2026.
[25] Ibid.
[26]Consideration of the Emergency Situation in Libya, Amani Africa Insights on the (AU) Peace and Security Council, 22 May 2025 – imefikiwa tarehe 22 Machi 2026; angalia pia Communiqué,

22. Jambo la kuangalia hasa, katika hali hizi nyingi, uwajibikaji kutokana na ukiukaji mkubwa na wa hali ya juu wa haki za binadamu na watu bado haujatekelezwa. Kuendelea kufanywa kwa ukiukaji kama huo kumesababisha mateso yasiyoelezeka miongoni mwa watu wa Afrika, kunatishia uwepo wao, kunazuia na kudhoofisha kwa kiasi kikubwa maendeleo yao ya kijamii na kiuchumi na kitamaduni. Kama inavyothibitishwa na mifano iliyoangaziwa hapo juu, hali ya sasa ya amani, usalama na haki za binadamu barani Afrika inahatarisha kufanikiwa kwa matarajio ya Ajenda ya 2063 iliyotajwa hapo juu. Ikiwa matarajio haya yanapaswa kufikiwa, ni muhimu kwamba Mataifa ya Afrika, nchi moja moja na kwa pamoja, yajizatiti tena kuzuia kujirudia, na kuhakikisha uwajibikaji, kwa ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu na watu barani kote.

23. Kwa hivyo, Ombi hili la Maoni ya Ushauri linaialika Mahakama hii tukufu katika kutekeleza mamlaka yake chini ya Mkataba wa Afrika na Itifaki ya Mahakama ya Afrika ili kuyafafanulia Mataifa wanachama, wigo wa wajibu wao wa kulinda na kutetea haki za binadamu, hasa kuhusiana na uwajibikaji kwa ukiukaji mkubwa au ukatili wa halaiki unaofikia kiwango cha ukiukaji mkubwa na wa halaiki wa haki za binadamu chini ya Kifungu cha 58 cha Mkataba wa Afrika. Kwa umahususi, Ombi hili linalenga kupata ufafanuzi rasmi kutoka kwenye Mahakama kuhusu wajibu wa kisheria wa Mataifa ya Afrika kuhusiana na uwajibikaji wa makosa ya jinai ya mtu binafsi kwa ukiukaji mkubwa, wa kiwango kikubwa au ukiukaji mbaya sana wa haki za binadamu na watu, kama sehemu ya wajibu wa Nchi wanachama.

## V. SHERIA INAYOTUMIKA

24. Sheria ya msingi ambayo Ombi hili limejikita ni Mkataba wa Afrika. Ombi hili linalenga kupata ufafanuzi wa aya za 10 na 11 za utangulizi na Kifungu cha

Peace and Security Council (PSC) of the African Union (AU) at its 1280th meeting held on 23 May 2025 on the Situation in Libya, PSC/PR/COMM.1280(2025), (23 Mei 2025) – imefikiwa tarehe 20 Aprili 2026.

1 na 58 cha Mkataba wa Afrika kuhusiana na kujizatiti kwa nchi wanachama, nchi moja moja na kwa pamoja, kutimiza wajibu wao wa kulinda na kutetea haki za binadamu na watu zilizowekwa ndani yake.

25. Ombi hili pia linawasilisha, kama nyenzo saidizi ya ufafanuzi wa masharti husika ya Mkataba wa Afrika, mikataba mingine husika ambayo Nchi za Afrika ni wanachama, na sheria ya kidesturi ya kimataifa. Bila kuweka mipaka, masharti haya yanajumuisha:

a) Vifungu vya 2(1) na (3) vya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa.

b) Vifungu vya 4, 5, 7 na 8 vya Mkataba dhidi ya Mateso na Matendo au Adhabu Nyingine za Kikatili, Kinyama au Kudhalilisha.

c) Vifungu vya 9 na 11 vya Mkataba wa Kimataifa wa Ulinzi wa Watu Wote dhidi ya Kuwekwa Kizuizini kwa Siri (2006).

d) Vifungu vya 2(2) na 4 vya Itifaki ya Mkutano wa Kimataifa wa Maziwa Makuu kuhusu Kuzuia na Kukomesha Ukatili wa Kingono dhidi ya Wanawake na Watoto, 2006.

e) Vifungu vya I na VI vya Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari.

f) Vifungu vya 3(h) na 25(d) vya Itifaki ya A/P.1/12/99 Kuhusu Utaratibu wa Kuzuia, Kudhibiti, Kutatua Migogoro, Kulinda Amani na Usalama (Itifaki ya Lomé).

g) Vifungu vya 8, 9, 10, 11 na 11 vya Itifaki ya Mkutano wa Kimataifa wa Maziwa Makuu ya Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari, Uhalifu wa Kivita na Uhalifu dhidi ya Binadamu na aina zote za Ubaguzi, 2006.

h) Vifungu vya 3(h) na 4(h) vya Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika.

i) Vifungu vya 4(g) na 56(2) vya Mkataba Uliorekebishwa wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi, 1993.

j) Kifungu cha 3 cha Mkataba Uliorekebishwa wa Umoja wa Kiuchumi na Kifedha wa Afrika Magharibi (Traité Modifié de l'Union Economique et Monétaire Ouest Africaine).

k) Ibara ya 5(3)(f), 6(d) na 7(2) ya Mkataba wa Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

l) Kifungu cha 4(c) cha Mkataba Uliojumuishwa wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika.

m) Vifungu vya 6(e), (f), (g) na (i) vya Mkataba wa Kuanzisha Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Kusini.

## VI. MASUALA YA KUAMUA

26. PALU inaomba kwa heshima kupata maoni ya Mahakama Tukufu kuhusu maswali yafuatayo:

a) Ndani ya vifungu vya pamoja vya Kifungu cha 1 na 58(1)-(2) cha Mkataba wa Afrika kama vilivyo, au vikisomwa pamoja na Kifungu cha 3(h) na 4(h) cha Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, endapo kuna wajibu kwa Nchi Wanachama wa kuzuia ukiukaji mkubwa na wa kiasi kikubwa wa haki za binadamu na, pale unapotokea, kuhakikisha uwajibikaji wa uhalifu kwa ukiukaji huo.

b) Kutokana na mwingiliano kati ya Mkataba wa Afrika na Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, ni kwa kiwango gani wajibu wa Nchi za Afrika yanajumuisha wajibu wa kuhakikisha uwajibikaji wa jinai, ikiwemo kupitia uanzishwaji wa mifumo madhubuti ya ushirikiano wa kikanda?

c) Iwapo wajibu uliokubaliwa na Nchi Wanachama wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu chini ya Kifungu cha 1 cha Mkataba huo

"kuchukua hatua za kisheria au nyinginezo ili kutekeleza" masharti ya Mkataba huo haujumuishi wajibu wa kutenda kwa kujitegemea na kwa kushirikiana na nchi nyingine, kuhakikisha uwajibikaji unafanywa kwa ufanisi kwa mtu binafsi kutokana na ukiukaji mkubwa na wa kiasi kikubwa wa haki za binadamu na watu barani Afrika.

d) Kwa kuzingatia masharti ya Mkataba wa Afrika na hati zingine za kisheria zinazotumika, ni majukumu gani ya kisheria, ikiwa yapo, ambayo Mataifa ya Afrika yanayo kuweza kuanzisha na kutekeleza mifumo madhubuti ya ushirikiano, iwe kupitia Umoja wa Afrika, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda za Afrika (REC) au mifumo mingine husika ya kikanda, ili kuhakikisha uwajibikaji wa jinai kwa watu wanaodaiwa kufanya ukiukaji mkubwa au wa kiasi kikubwa wa haki za binadamu na watu barani humo?

e) Aidha, ni matokeo gani ya kisheria yanayofuata kutokana na Nchi za Afrika kukataa au kushindwa, zikitenda kwa kujitegemea au kwa pamoja kupitia Umoja wa Afrika au Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda za Afrika, kumkabidhi mtu kwa nchi nyingine au kumshitaki mtu anayeshukiwa kufanya ukiukaji mkubwa na wa kiasi kikubwa wa haki za binadamu na watu barani Afrika?

## VII. MUHTASARI WA HOJA: WAJIBU NA VIWANGO VYA KISHERIA VINAVYOTUMIKA

### *A. Maana, maudhui na wigo wa ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya sana wa haki za binadamu na za watu*

27. Uamuzi wa swali la kwanza lililoulizwa utaamua uamuzi wa Ombi lote. Ili kuisaidia Mahakama kujibu swali la kwanza lililoulizwa, PALU inaona inafaa kuwasilisha maana, maudhui na wigo wa kirai "ukiukaji mkubwa au wa hali ya juu wa haki za binadamu na watu" chini ya Kifungu cha 58(1) cha Mkataba wa Afrika.

28. Mfumo wa kisheria wa bara la Afrika unatambua kwamba ukiukaji fulani wa haki za binadamu na za watu unaweza kuwa na asili "maalumu" kiasi cha kuhitaji majibu ya kipekee. Kwa mfano, Kifungu cha 58 cha Mkataba wa Afrika kinatoa fursa ya uingiliaji kati usio na kifani wa Tume ya Afrika na Baraza la Umoja wa Afrika katika "kesi maalumu zinazoonyesha kuwepo kwa mfululizo wa ukiukaji mkubwa au wa hali ya juu wa haki za binadamu na za watu". Mkataba wa Afrika hauelezi "ukiukaji mkubwa au wa hali ya juu wa haki za binadamu na watu." Hata hivyo, maana ya jumla ya kile kinachojumuisha "ukiukaji mkubwa au wa hali ya juu wa haki za binadamu na za watu" inaweza kutambuliwa kutokana na utendaji wa mashirika ya Umoja wa Afrika.

29. Kanuni ya 2 ya Kanuni za Utaratibu wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ("Tume ya Afrika"), 2020 inafafanua ukiukaji mkubwa au wa hali ya juu kuwa "ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu unaotambulika kwa kiwango na umuhimu wake." Ingawa fasili hii haitoi uelewa wa kutosha kuhusu asili halisi ya "ukiukaji mkubwa au wa hali ya juu," utendaji na busara ya kisheria ya Tume ya Afrika hutoa mwongozo fulani, angalau kuhusiana na aina mahususi za ukiukaji ambazo zingekuwa kwenye kundi hili.

30. Katika Mawasiliano namba 27/89-46/91-49/91-99/93,[27] Tume iliona kwamba "mauaji ya watu wengi, mauaji ya kinyama na ukamataji usio na misingi dhidi ya kabila la Watutsi" ulikuwa ukiukaji mkubwa au wa hali ya juu. Matokeo kama hayo yameonyeshwa na Tume kuhusiana na "ripoti kadhaa za mauaji, kutoweka na mateso" ikiwemo katika Mawasiliano namba 74/92,[28] kuhusu kuwekwa kizuizini kwa watu wengi bila kupelekwa mahakamani, mateso ya kiwango kikubwa magerezani, mauaji bila hukumu

[27]Mawasiliano namba 27/89-46/91-49/91-99/93, Organisation mondiale contre la torture, Association Internationale des juristes démocrates, Commission internationale des juristes, Union interafricaine des droits de l'Homme dhidi ya Rwanda (tarehe 31 Oktoba 1996) aya ya 4 na 16.
[28]Mawasiliano namba 74/92, Commission nationale des droits de l'Homme et des libertés dhidi ya Chadi (tarehe 11 Oktoba 1995).

ya mahakama na mauaji ya maelfu ya raia nchini Chad;[29] na Mawasiliano na 279/03-296/05[30] kuhusu mauaji ya kiwango kikubwa, watu kupotezwa, uharibifu wa majengo ya umma, mali na kuvuruga utaratibu wa maisha kupitia mabomu yaliyotupwa na ndege za kivita katika maeneo yenye watu wengi, mauaji bila hukumu ya mahakama, mateso, ubakaji wa wanawake na wasichana, ukamataji kiholela na kufungwa nchini Sudan.

31. Maazimio na ripoti za Tume ya Afrika pia hutoa mwongozo zaidi kuhusu kile inachokiona kuwa ukiukaji mkubwa au wa hali ya juu. Katika Azimio lake la 1994 ACHPR/Res.8(XV)94 kuhusu Hali nchini Rwanda, Tume ililaani "mauaji ya raia wasio na hatia"[31] wanapoelezea wasiwasi wao kuhusu ukiukwaji mkubwa na wa hali ya juu wa haki za binadamu.[32] Vivyo hivyo katika Azimio lake la mwaka 2005 ACHPR/Res.74(XXXVII)05 kuhusu Hali ya Haki za Binadamu huko Darfur, Sudan, Tume iliwahimiza wahusika wa mzozo kusitisha "mashambulizi dhidi ya raia huko Darfur … kampeni ya kuwafukuza watu kwa nguvu kutoka maeneo yote … mashambulizi ya ovyo dhidi ya vijiji, ubakaji na ukatili wa kingono dhidi ya wanawake, wasichana na watoto, utekaji nyara wa wanawake na watoto, uporaji wa mifugo na vyakula kwenye vijiji".[33] Azimio la mwaka 2010 la ACHPR/Res.173(XLVIII)10 kuhusu Uhalifu Uliofanywa Dhidi ya Wanawake nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo lililaani "vitendo vilivyofanywa kwa njia iliyopangwa na vilivyoenea sana vya ubakaji unaofanywa na makundi yenye silaha dhidi ya wanawake na wasichana wadogo hasa

[29]Angalia pia Mawasiliano namba 48/90-50/91-52/91-89/93, Amnesty International, Comité Loosli Bachelard, Kamati ya Wanasheria ya Haki za Binadamu, Chama cha Wajumbe wa Baraza la Maaskofu la Afrika Mashariki dhidi ya Sudani (tarehe 15 Novemba 1999).
[30]Mawasiliano namba 279/03-296/05, Shirika la Haki za Binadamu la Sudan na Kituo cha Haki za Makazi na Kufukuzwa (COHRE) dhidi ya Sudan (tarehe 27 Mei 2009).
[31]Azimio namba ACHPR/Res. 8(XV) 94 kuhusu Hali nchini Rwanda (tarehe 27 Aprili 1994), aya ya 1.
[32]Azimio namba ACHPR/Res. 8(XV) 94 kuhusu Hali nchini Rwanda (tarehe 27 Aprili 1994), utangulizi.
[33]Azimio namba ACHPR/Res.74(XXXVII)05 kuhusu Hali ya Haki za Binadamu huko Darfur, Sudan (tarehe 11 Mei 2005), aya ya iii; angalia pia Azimio la ACHPR/Res.68 (tarehe 4 Juni 2004).

katika eneo la Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo",[34] ilhali Azimio la mwaka 2016 la ACHPR/Res. 357(LIX)2016 kuhusu Hali ya Haki za Binadamu nchini Burundi lilionyesha wasiwasi kuhusu "ukamataji wa mara kwa mara na kuwekwa kizuizini kiholela, mauaji ya kulenga watu mahususi, mauaji bila hukumu ya mahakama, vitendo vya mateso na aina nyingine vitendo vya kikatili, visivyo vya kibinadamu na vya kudhalilisha, utekaji nyara na kupotezwa, uonevu na vitisho dhidi ya waandishi wa habari na wanahabari, ukatili wa kingono na aina nyingine za ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu."[35]

32. Kwa kutilia maanani, Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu inatumia maneno tofauti kidogo na Mkataba wa Afrika, ikielezea katika Kifungu cha 27(2) kwamba, "Katika hali mbaya sana na ya dharura, na inapohitajika ili kuepuka madhara kwa watu yasiyoweza kurekebishwa, Mahakama itachukua hatua hizo za muda kama inavyoona kuwa ni lazima." Katika Kesi ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu dhidi ya Jamahiriya ya Kiarabu ya Wasosholisti wa Libya,[36] kufuatia hitimisho la Tume ya Afrika kwamba ukandamizaji wa waandamanaji kwa nguvu uliofanywa na vikosi vya usalama uliopelekea mauaji na majeraha na mashambulizi dhidi ya raia ikiwemo mashambulizi ya anga, yalikuwa ukiukaji mkubwa na wa hali ya juu wa haki za binadamu, Mahakama ya Afrika iliamua kwamba mambo haya pia yalikuwa hali ya uzito mkubwa na ya dharura. Vivyo hivyo, katika kesi ya Bernard Anbataayela Mornah dhidi ya Jamhuri ya Benin na Wengine 7, Mahakama iliamua kwamba madai ya ukiukaji wa miongo kadhaa wa uhuru wa mamlaka, uhuru wa kieneo, uhuru

[34]Azimio namba ACHPR/Res.173(XLVIII)10 kuhusu Uhalifu Uliofanywa dhidi ya Wanawake katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (tarehe 24 Novemba 2010).
[35]Azimio la ACHPR/Res. 357(LIX)2016 kuhusu Hali ya Haki za Binadamu nchini Burundi (tarehe 4 Novemba 2016).
[36]Maombi Na. 004/2011, Amri ya Hatua za Muda, tarehe 25 Machi 2011, aya za 10–13 na 22.

wa kisiasa, haki ya amani na kujitawala ni ukiukaji mkubwa na mbaya wa haki za binadamu.[37]

33. Mamlaka zaidi ya ushawishi ni pamoja na ripoti za vyombo mbalimbali vya Umoja wa Afrika, ikiwemo Ripoti ya mwaka 2004 ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Ujumbe wa Kutafuta Ukweli kwenda Jamhuri ya Sudan, ambao ulibaini kwamba wahusika wa mzozo walikuwa wamefanya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu ikiwemo mauaji yaliyoenea sana na ya kimfumo, mashambulizi na mabomu dhidi ya raia na vijiji, ubakaji na uhamishaji wa watu wengi, na ambapo ripoti hiyo iliona pia kuwa ni uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu.[38]

34. Vilevile, mamlaka ya Tume ya Uchunguzi ya Umoja wa Afrika kuhusu Sudan Kusini (AUCISS) kulingana na hati zake za mwongozo yalijumuisha kuchunguza "ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu,"[39] ambao AUCISS iliufasiri kuwa unajumuisha uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu, ambao ndio ukawa ndio mwelekeo wa ripoti yake ya mwaka 2014.[40] Mifano ya ziada inajumuisha Ripoti ya Ujumbe wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kuhusu Ujumbe wake wa Uchunguzi wa Ukweli nchini Burundi, ambayo pia ilirekodi ukiukaji mkubwa na wa hali ya juu wa haki za binadamu ikiwemo mauaji ya halaiki ya waandamanaji, mauaji bila hukumu na mauaji yanayofanywa na vikosi vya usalama katika kipindi kilichofuatia maandamano na mamia ya visa vya mateso yanayofanywa na vyombo vya

---

[37] Bernard Anbataayela Mornah dhidi ya Jamhuri ya Benini na Wengine 7 [Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiarabu ya Sahrawi na Jamhuri ya Moishasi: Waingiliaji kati], Maombi Na. 028/2018, Hukumu, tarehe 22 Septemba 2022, aya ya 211.

[38] Ripoti ya Ujumbe wa Kutafuta Ukweli wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwenda Jamhuri ya Sudan katika Eneo la Darfur (tarehe 8–18 Julai 2004) EX.CL/364 (XI) Kiambatisho cha III, aya za 120–123.

[39] Ripoti ya Mwisho ya Tume ya Uchunguzi ya Umoja wa Afrika kuhusu Sudan Kusini (tarehe 15 Oktoba 2014) <https://www.peaceau.org/uploads/auciss.final.report.pdf>, aya ya 3.

[40] AUCISS iliona kwamba uhalifu dhidi ya binadamu 'kimsingi ni ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu, wakati mwingine hujulikana kama ukiukaji wa hali ya juu wa haki za binadamu'. Angalia Ripoti ya Mwisho ya Tume ya Uchunguzi ya Umoja wa Afrika kuhusu Sudan Kusini (tarehe 15 Oktoba 2014) <https://www.peaceau.org/uploads/auciss.final.report.pdf>, aya ya 379.

usalama.[41] Vivyo hivyo, Azimio la Tume ya Afrika ACHPR/Res. 482 (EXT.OS/XXXII) 2021 ambalo lilianzisha Ujumbe wa Uchunguzi wa Ukweli katika Mkoa wa Tigray wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia liliona "ukiukaji mkubwa" unajumuisha "unyanyasaji wa kingono dhidi ya wanawake na wasichana, ubakaji wa kundi unaotumiwa kama silaha za vita, mauaji ya raia yanayofanywa na wapiganaji na mauaji bila hukumu ya mahakama."[42]

35. Sera ya Haki ya Mpito ya Umoja wa Afrika, 2019 (AUTJP) hutumia maneno "ukiukaji wa kimfumo au wa hali ya juu wa haki za binadamu na za watu" na "ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu" kwa kubadilishana. Kwa kutilia maanani, AUTJP inasisitiza kwamba "ukiukaji mkubwa, hasa ule uliotajwa chini ya Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, ikiwemo ukiukaji wa kingono na wa kijinsia" lazima uchunguzwe kikamilifu na kushtakiwa[43] na kwamba msamaha usio na masharti haupaswi kupatikana kwa wale wanaoshukiwa kufanya ukiukaji huu.[44] Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, kama ilivyorejelewa kwenye AUTJP, kinahusu "hali mbaya, yaani: uhalifu wa kivita, mauaji ya kimbari na uhalifu dhidi ya binadamu." Kwa hivyo, hii inamaanisha kwamba AUTJP inaona "ukiukaji mkubwa au mbaya" kuwa unajumuisha, angalau, uhalifu wa kivita, mauaji ya kimbari na uhalifu dhidi ya binadamu. AUTJP inahitaji zaidi kwamba kusiwe na kikomo kwenye uchunguzi kamili na mashtaka ya ukiukaji mkubwa, hasa ule uliotajwa chini ya Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, ikiwemo ukiukaji wa kingono na wa kijinsia. Kanuni ni kwamba mashtaka yanapaswa kusababisha hukumu na kutoa adhabu ambayo kwa kawaida hutumika katika michakato ya jinai ya kitaifa na kimataifa na kufuata mchakato unaofaa wa sheria.

[41]Ripoti ya Ujumbe wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kazi yake ya Kutafuta Ukweli nchini Burundi, tarehe 7–13 Desemba 2015, aya za 110–126.
[42]Azimio namba ACHPR/Res. 482 (EXT.OS/XXXII) 2021 (tarehe 12 Mei 2021), utangulizi.
[43]Sera ya Haki ya Mpito ya Umoja wa Afrika (Februari 2019), aya ya 86.
[44]Sera ya Haki ya Mpito ya Umoja wa Afrika (Februari 2019), aya ya 91.

36. Kwa hivyo, kirai "ukiukaji mkubwa au wa hali ya juu wa haki za binadamu na za watu"[45] si kigeni katika msamiati wa haki za binadamu wa Afrika; kimsingi kinatumika sana kwenye vyombo vya Umoja wa Afrika. Kwa madhumuni ya Ombi hili, PALU inasema kwamba kirai hiki kinamaanisha vipengele vya viwango na vya kitakwimu mtawalia. Kwa maneno mengine, kinaweza kujumuisha vigezo vinavyotegemea uzito wa vitendo hivyo na asili yake ya kimfumo au ya kiwango kikubwa kama msingi wa kuamua kinachojumuisha "ukiukaji mkubwa au wa hali ya juu wa haki za binadamu na watu." Pia kinaeleweka kuwa kinajumuisha ukiukaji ambao ni sawa na uhalifu wa kimataifa uliofasiliwa vizuri, ikiwemo ule uliotajwa katika Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya Kikatiba, ambacho kinatoa fursa ya uingiliaji kati usio na kifani wa Umoja wa Afrika. Kwa hivyo, angalau, ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya sana wa haki za binadamu na za watu unapaswa kuangaliwa kuwa unajumuisha ukiukaji ule ambao ni sawa na uhalifu wa kimataifa, kama vile uhalifu wa kivita, mauaji ya kimbari, uhalifu dhidi ya binadamu au mateso.

37. Aidha, PALU inawasilisha kwamba kujitokeza kwa kifungu hiki katika nyaraka mbalimbali ni dalili ya kuwepo kwa opinio juris. Hii inamaanisha kuwa mataifa yanachukulia tabia hiyo kuwa ya lazima kisheria. Vilevile, mazoea yanayolingana nayo yanaonyesha tabia ya nchi ambayo, pamoja na opinio juris, ni sehemu mbili muhimu katika kutambulisha sheria za kimila za kimataifa (katika muktadha wa Afrika) kuhusu wajibu wa kuchukua hatua kukabiliana na ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu na watu. Kisha jambo linalofuata linalopaswa kuzingatiwa linahusu njia mahususi za wajibu.

***B. Wajibu wa kuchunguza na kufungua mashtaka***

[45] Virai 'ukiukaji mkubwa au wa hali ya juu wa haki za binadamu na watu' na 'ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu na watu' vinaweza kutumika kwa kubadilishana katika Ombi hili.

38. Kwa kujibu maswali yaliyoulizwa kwenye MASUALA YA KUAMUA hapo juu, PALU inawasilisha kwamba Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika, kikifasiriwa kwa makusudi: –

a) kinaweka wajibu kwa Nchi za Afrika kila moja kivyake kuchunguza na kufungua mashtaka dhidi ya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na za watu;

b) kinaweka wajibu kwa Nchi za Afrika kwa pamoja chini ya uundaji wa Umoja wa Afrika kuingilia kati, ikiwemo kutumia mifumo ya uwajibikaji wa jinai, katika hali za ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu, na

c) kinaweka wajibu kwa Nchi za Afrika kwa pamoja ndani ya mifumo ya taasisi kama vile Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (REC) kushirikiana ili kuhakikisha uchunguzi na kufungua mashtaka dhidi ya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu barani Afrika.

39. PALU inawasilisha kwamba sheria ya kimataifa kwa ujumla, na sheria ya kimataifa ya haki za binadamu kwa umahususi, huweka wajibu kwa Mataifa ya Afrika kuhakikisha kuna kuwa na uwajibikaji wa jinai kutokana na ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu. Wajibu huu unatokana na Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika, kutoka kwenye vifungu vya mikataba mingine ya haki za binadamu ambayo inaweka sheria za haki na wajibu unaoambatana nazo, pamoja na kutoka kwenye sheria ya kidesturi ya kimataifa.

40. Aidha inawasilisha kwamba sasa ni kanuni iliyowekwa katika sheria ya kimataifa kwamba Mataifa yana wajibu wa kuchunguza na kufungua mashtaka dhidi ya ukiukaji mkubwa, wa kiwango kikubwa au mbaya wa haki za binadamu na watu; huu ni msimamo unaoongozwa na tafsiri yenye mamlaka ya mahakama za kimataifa kuhusu wajibu wa Mataifa chini ya

mikataba mbalimbali iliyotajwa hapo juu,[46] ambayo tafsiri yake inasisitiza uchunguzi, mashtaka na adhabu ya ukiukaji huu kama wajibu wa msingi wa Mataifa.

41. Wajibu wa jinai kwa ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu kwa ujumla unategemea wajibu wa kuheshimu, kuhakikisha na kutekeleza haki na uhuru wa msingi na kutoa suluhu madhubuti kwa ukiukaji, kama ilivyoainishwa wazi katika mikataba mbalimbali ya haki za binadamu ukiwemo Mkataba wa Afrika.

42. Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika kinawawajibisha Nchi Wanachama "kutambua haki, majukumu na uhuru uliowekwa katika Mkataba huu na […] kutumia hatua za kisheria au nyinginezo ili kuzitekeleza." Mifumo ya kimahakama na inayofanya maamuzi kama ya kimahakama ya Afrika imetafsiri Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika, ambacho kinatoa wajibu kwa Nchi Wanachama kutekeleza haki na uhuru, kuwa kinajumuisha wajibu wa kuchunguza na kufungua mashtaka dhidi ya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu. Kwa maneno mengine, ingawa haijaelezwa waziwazi hivyo katika Mkataba wa Afrika, mifumo hii imetafsiri na kufafanua kwa mamlaka asili, maudhui na wigo wa Kifungu cha 1 cha Mkataba kama kinavyosomwa pamoja na haki za msingi zilizotajwa waziwazi ndani yake, na kuhitimisha kwamba vifungu hivi vinajumuisha wajibu wa kiutaratibu wa kuchunguza kwa ufanisi na kufungua mashtaka dhidi ya ukiukaji wa haki hizi za msingi ili kuimarisha kiini chake na kuhakikisha ulinzi mkubwa.[47] Busara ya kisheria ya Tume ya Afrika zinaendana na kifungu hiki.

[46] Angalia pia Owiso Owiso, '"Obligation to Strangers": Reconceptualizing Cosmopolitanism as a Basis for Collective (Regional-Level) Accountability for International Crimes' 21(1) Journal of International Criminal Justice 1 (2021).
[47] Ezéchiel Amani Cirimwami, 'Fashioning Rights in the African Court on Human and Peoples' Rights: Understanding the Proceduralisation of Substantive Rights' (2020) 4 African Human Rights Yearbook 1, 5–11.

43. Katika kesi ya Zimbabwe Human Rights NGO Forum dhidi ya Zimbabwe,[48] Tume ilithibitisha kwamba wajibu wa kufanya uchunguzi makini wa ukiukaji wa haki zinazolindwa chini ya sheria ya kimataifa, kutambua wahusika na kutoa adhabu inayofaa, ni kipengele cha msingi cha wajibu wa Mataifa chini ya Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika, yaani kutambua na kutekeleza haki, aidha, kwamba uthibitisho huu "unawakilisha tafsiri yenye mamlaka ya kiwango cha kimataifa kuhusu wajibu wa Serikali." Kwa kutilia maanani, Tume ya Afrika ilisukumwa na hukumu maarufu ya Mahakama ya Bara la Amerika ya Haki za Binadamu (Mahakama ya Bara la Amerika) katika kesi ya Velásquez (hapa chini).

44. Msimamo huu pia umethibitishwa mara kwa mara na Tume ya Afrika katika hukumu zilizofuata, ikiwemo katika kesi ya Dino Noca dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo[49] ambapo Tume iliamua kwamba, "Ni wajibu wa Nchi kuchunguza na kurekebisha ukiukaji chini ya wajibu wa jumla unaowapasa kwa mujibu wa Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu."

45. Mahakama hii Tukufu katika hukumu yake ya mwaka 2014 katika Kesi ya Zongo,[50] vile vile ilitafsiri Kifungu cha 1 (wajibu wa kutambua na kutekeleza haki) na 7 cha Mkataba wa Afrika (wajibu wa mtu kusikilizwa na mahakama husika za kitaifa) kama wajibu wa Serikali kufanya uchunguzi wa haraka na wenye ufanisi na kuwafungulia mashtaka na "kuwafikisha mahakamani" wale wanaohusika na ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu kama vile mauaji.

---

[48]Mawasiliano namba 245/02, yaliyopitishwa katika Kikao cha Kawaida cha 39 kilichofanyika kuanzia tarehe 11–15 Mei 2006, aya za 142–144.
[49]Mawasiliano namba 286/2004, yaliyopitishwa katika Kikao cha Kawaida cha 52 kilichofanyika kuanzia tarehe 09–22 Oktoba 2012, aya ya 158; angalia pia IHRDA et autres c République Démocratique du Congo, Mawasiliano namba 700/18, yaliyopitishwa katika Kikao cha Kawaida cha 80 kilichofanyika kuanzia tarehe 24 Julai–02 Agosti 2024 – imefikiwa tarehe 12 Agosti 2025.
[50]Wanufaika wa marehemu Norbert Zongo, Abdoulaye Nikiema anayejulikana kama Ablassé, Ernest Zongo na Blaise Ilboudo na mwingine dhidi ya Burkina Faso, Maombi Na. 013/2011, Hukumu, tarehe 28 Machi 2014, aya ya 150–156 na 198–199.

46. Kina cha busara hii ya kisheria pia kinathibitishwa na matumizi yake katika mifumo ya kikanda. Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (Mahakama ya ECOWAS) pia imepitisha msimamo huo hapo juu. Katika uamuzi wake wa mwaka 2024 katika kesi ya Global Justice and Research Project na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Liberia, Mahakama ya ECOWAS ilitafsiri waziwazi Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika kama kuweka wajibu kwa Nchi Wanachama "kuheshimu, kulinda, kutetea na kutimiza haki zilizowekwa katika Mkataba"[51] na kwamba "chini ya wajibu huu, Mataifa yana wajibu wa kuchunguza vitendo vyote vya uhalifu na kuwashtaki wahusika wote".[52]

47. Katika uamuzi wa awali katika kesi ya Hadijatou Mani Karaou dhidi ya Jamhuri ya Niger,[53] Mahakama ya ECOWAS iliamua kwamba kushindwa kwa Niger kulaani, kuzuia na "kuhakikisha kwamba mashtaka yanafunguliwa au kwamba adhabu zilipendelewa" kulikuwa sawa na kuvumilia kimyakimya, jambo ambalo kwa upande wake lilikiuka wajibu wake wa kuhakikisha kwamba kuna njia zenye ufanisi za kutafuta haki na kudumisha marufuku ya utumwa chini ya sheria za kimataifa na za ndani. Vivyo hivyo, katika kesi ya Oluwatimilehin Adebayo dhidi ya Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria[54] Mahakama ya ECOWAS ilithibitisha kwamba kushindwa kwa Serikali, licha ya kufahamu kuwepo kwa ukiukaji wa haki za binadamu (hasa, mateso), kutofanya uchunguzi wa haraka, usio na upendeleo na wenye ufanisi kuhusu ukiukaji huu, kutambua wahusika na

[51] ECW/CCJ/APP/48/22; ECW/CCJ/RUL/04/24 [2024] ECOWASCJ 19 (tarehe 17 Oktoba 2024), aya ya 44 – ilifikiwa tarehe 12 Agosti 2025.
[52] Ibid., aya ya 45.
[53] Mahakama ya Jumuiya ya Haki, Ripoti za Sheria za ECOWAS (2004–2009 CCJELR) uk. 217–244, ECW/CCJ/APP/08/08; ECW/CCJ/JUD/06/08 (tarehe 27 Oktoba 2008), aya ya 81–86.
[54] ECW/CCJ/APP/47/23; ECW/CCJ/JUD/44/24 [2024] ECOWASCJ 25 (tarehe 3 Desemba 2024), aya za 91–96. Angalia pia Dorothy Chioma Njemanze na wengine 2 dhidi ya Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria, Ripoti za Sheria za ECOWAS (2017 CCJELR) ukurasa wa 139–176, ECW/CCJ/APP/17/14, ECW/CCJ/JUD/08/17 (tarehe 12 Oktoba 2017) ukurasa wa 173–176; Hembadoon Chia na wengine 7 dhidi ya Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria na mwingine, ECW/CCJ/APP/07/16, ECW/CCJ/JUD/21/18, [2018] ECOWASCJ 21 (tarehe 29 Juni 2018), ukurasa wa 30; The Registered Trustees of Jama'a Foundation na wengine 5 dhidi ya Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria na mwingine, ECW/CCJ/APP/26/13, ECW/CCJ/JUD/04/20 (tarehe 20 Machi 2020), aya ya 115–119 na 122 – ilifikiwa tarehe 14 Agosti 2025.

kutoa haki kwa kuwawajibisha wahusika, kutakuwa ukiukaji chini ya sheria ya kimataifa ikiwemo Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika na Kifungu cha 13 cha Mkataba dhidi ya Mateso. Baadaye Mahakama iliiamuru Nigeria "ifanye uchunguzi wa haraka, usio na upendeleo na wenye ufanisi … na kuwafungulia mashtaka na kuwafikisha mbele ya sheria wahusika wote."[55]

48. Kuhusiana na wajibu wa kuchunguza na kushtaki, ni muhimu kutambua kwamba Mahakama ya ECOWAS iliamua katika kesi ya Global Justice and Research Project na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Liberia, ambayo ilihusu kushindwa kwa Liberia kuchunguza na kufungua mashtaka dhidi ya ukiukaji mkubwa na mbaya wa haki za binadamu uliotokana na mauaji ya halaiki kanisani mwaka 1990, na ambapo kushindwa huko Waleta Maombi walidai kulikiuka Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika, kwamba kutafuta suluhu kutokana na ukiukaji wa haki za binadamu, hasa ule mbaya na wa hali ya juu, hakuwezi kuwa na vikomo vya muda.[56]

49. Kwa hivyo ni dhahiri kwamba katika mfumo wa haki za binadamu wa Afrika, kuna kutambua kwamba "kutokuwepo [kwa mashtaka ya jinai] kunajumuisha ukiukaji wa serikali kushindwa kutekeleza wajibu wake wa kulinda haki za mkataba".[57] Aidha, pia inatambuliwa "kwamba ni mashtaka dhidi ya jinai yenye ufanisi na ufasaha pekee ndiyo yanayoweza kuwalinda watu dhidi ya ukiukaji usiovumilika wa haki zao zilizowekwa na Mkataba."[58] Inawasilishwa kwamba misimamo hii inatumika kwa nguvu zaidi hata kwa ukiukaji mkubwa au wa kikatili wa haki za binadamu na watu. Msimamo huu unaendana kabisa na ule uliopitishwa na mifumo mingine ya haki za binadamu.

[55]Ibid., xi (kifungu cha utekelezaji).
[56]Supra, fn 45 hapo juu, aya za 23–24.
[57]Ezéchiel Amani Cirimwami, 'Fashioning Rights in the African Court on Human and Peoples' Rights: Understanding the Proceduralisation of Substantive Rights' (2020) 4 African Human Rights Yearbook 1, 9.
[58] Id.

50. Vilevile, katika hukumu yake maarufu ya mwaka 1988 katika kesi ya Velásquez Rodríguez dhidi ya Honduras, Mahakama ya Bara la Amerika ilitafsiri Kifungu cha 1(1) cha Mkataba wa Amerika wa Haki za Binadamu, ambacho kinaweka wajibu kwa Nchi Wanachama kuheshimu na kuhakikisha utekelezaji huru na ulio kamili wa haki, kama wajibu thabiti kwa Mataifa kuzuia ukiukaji wa haki za binadamu, kufanya uchunguzi makini dhidi ya ukiukaji na kuhakikisha kwamba wahusika wanaadhibiwa.[59] Msimamo huu umesisitizwa mara kadhaa tangu wakati huo na Mahakama ya Bara la Amerika katika kesi zinazohusisha ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu, ikiwemo hukumu yake ya mwaka 2005 katika Kesi ya Jumuiya ya Moiwana dhidi ya Surinamu, ambapo Mahakama ilisisitiza kwamba, kama suluhu za msingi za kisheria, Mataifa yana wajibu wa kufanya uchunguzi wa haraka, wenye umakini, wenye ufanisi na wa kina wa ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu na kutambua na kuwashtaki watu wanaowajibika kwa ukiukaji huo.[60]

51. Katika kufasiri wajibu unaofanana kwa kiasi kikubwa chini ya Kifungu cha 2(3) cha ICCPR wa kutoa suluhu yenye ufanisi, Kamati ya Haki za Binadamu katika Maoni ya Jumla ya 31 [80][61] kuhusu Hali ya Wajibu wa Kisheria wa Jumla kwa Nchi Wanachama wa Mkataba [kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa] ilithibitisha kwamba, kama kipengele cha msingi cha wajibu wa kuhakikisha suluhu kwa ukiukaji wa haki za binadamu, Nchi lazima zihakikishe zinafanya uchunguzi wa haraka, uchunguzi wa kina na wenye ufanisi na kuwafikisha wahusika mahakamani, kupitia uwajibikaji wa mtu binafsi (mhalifu), kwa ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu ikiwemo mateso, adhabu ya kikatili, isiyo ya kibinadamu na ya kudhalilisha, mauaji na kupotezwa, hasa yanapofanywa kama sehemu ya mashambulizi ya kiholela au ya kimfumo dhidi ya raia (yaani, uhalifu dhidi ya ubinadamu) na

---

[59]Mfululizo C Na. 4, Hukumu (Uzingatiaji wa Sheria), tarehe 29 Julai 1988, aya za 161–188.
[60]Mfululizo C Na. 124, Hukumu (Mapingamizi ya Awali, Uzingatiaji wa Sheria, Fidia na Gharama), tarehe 15 Juni 2005, aya za 144–147 – imefikiwa tarehe 15 Agosti 2025.
[61]Kamati ya Haki za Binadamu, Maoni ya Jumla 31 [80], CCPR/C/21/Rev.1/Add. 13 (2004), aya ya 15 na 18 – imefikiwa tarehe 15 Agosti 2025.

zaidi kwamba kushindwa kufanya hivyo ni ukiukaji mwingine wa wajibu wa kulinda haki za binadamu. Kwa maneno mengine, Kifungu cha 2(1) na (3) cha ICCPR, ambacho kinabainisha wajibu wa kuhakikisha, kuheshimu na kutoa suluhu ya kweli, kinatoa wajibu kwa Nchi kuchunguza na kufungua mashtaka dhidi ya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu.

52. Ufafanuzi huu wa wajibu wa Mataifa kuchunguza na kuwashtaki wahusika wa ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu pia tangu wakati huo umeonekana katika hati zingine za "sheria zisizo za lazima".

53. Kanuni za Msingi na Miongozo ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki ya Kupata Suluhu na Fidia kwa Wahanga wa Ukiukaji Mkubwa wa Sheria ya Kimataifa ya Haki za Binadamu na Ukiukaji Mkubwa wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, 2005 (Kanuni za Msingi) zinaweka msimamo kwamba Mataifa yana wajibu chini ya sheria ya kimataifa wa kutoa suluhu yenye ufanisi hasa kwa kuchunguza na kuwashtaki wahusika wa ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu na Kanuni ya 4 inaonyesha kwamba—

*Katika visa vya ukiukaji mkubwa wa sheria ya kimataifa ya haki za binadamu na ukiukaji mkubwa wa sheria ya kimataifa ya masuala ya kibinadamu unaojumuisha uhalifu chini ya sheria ya kimataifa, Mataifa yana wajibu wa kuchunguza na, ikiwa kuna ushahidi wa kutosha, wajibu wa kumfikisha mahakamani mtu anayedaiwa kuhusika na ukiukaji huo na, ikiwa atakutwa na hatia, wajibu wa kumwadhibu. Aidha, katika viza hivi, kwa mujibu wa sheria za kimataifa, Nchi zinapaswa kushirikiana na kusaidia vyombo vya kimataifa vya kimahakama vyenye uwezo wa kuchunguza na kushtaki ukiukaji huu.*

54. Rasimu ya Vifungu vya mwaka 2019 vya Tume ya Sheria ya Kimataifa kuhusu Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu dhidi ya Binadamu (Vifungu vya 3, 6,

7, 8, 9, 10 na 13) vinapendekeza wajibu kwa Nchi kuweka mamlaka ya kisheria juu ya, kuharamisha, kuchunguza, kuweka jinai na kuadhibu (kuwashtaki au kuwasafirisha washukiwa kwenda kushtakiwa nchi nyingine) uhalifu dhidi ya binadamu, huku Mkataba wa Ljubljana-The Hague wa mwaka 2023 kuhusu Ushirikiano wa Kimataifa katika Uchunguzi na Mashtaka dhidi ya Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari, Uhalifu dhidi ya Ubinadamu, Uhalifu wa Kivita na Uhalifu Mwingine wa Kimataifa (Vifungu vya 7 na 8) vivyo hivyo vinalenga kuweka wajibu kwa Nchi Wanachama kuharamisha na kuweka mamlaka ya kisheria ya jinai kuhusu mauaji ya kimbari, uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu.[62]

55. Pamoja na wajibu wa jumla wa kuheshimu na kuhakikisha haki, kama ilivyojadiliwa hapo juu, baadhi ya hati za kisheria pamoja na sheria ya kimataifa ya kidesturi huweka wajibu mahususi wa kisheria kwa Nchi kuhusiana na udhihirisho fulani wa ukiukaji mkubwa, wa kiwango kikubwa au mbaya wa haki za binadamu na watu, ikiwemo mauaji ya kimbari na mateso.

56. Mleta Maombi anadai kwamba Kifungu cha 4(1) cha Itifaki ya Mahakama ya Afrika kinatoa mamlaka kwa Mahakama hii Tukufu ya "kutoa maoni kuhusu suala lolote la kisheria linalohusiana na Mkataba au vyombo vingine vyovyote vya haki za binadamu." Kwa mujibu wa hati hii, Mahakama hii Tukufu, katika kujibu maswali yaliyoulizwa katika Ombi hili, inapaswa kuangalia mikataba mingine husika ambayo Nchi za Afrika ni wanachama, hasa vifungu vyake kuhusu udhihirisho mahususi wa ukiukaji mkubwa au wa hali ya juu wa haki za binadamu na za watu. Hii ni pamoja na:

a) Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari (Mkataba wa Mauaji ya Kimbari), Mkataba dhidi ya Mateso na Vitendo

---

[62] Ingawa si 'sheria isiyo ya lazima', Mkataba huo bado haujafikia idadi inayohitajika ya kuridhiwa ili uanze kutumika. Kufikia wakati wa Ombi hilo, hakuna Nchi ya Afrika iliyokuwa imeidhinisha mkataba huo.

au Adhabu Nyingine za Kikatili, Kinyama au Kudhalilisha (Mkataba dhidi ya Mateso);

b) Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa;

c) Itifaki ya Mkutano wa Kimataifa wa Maziwa Makuu ya Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari, Uhalifu wa Kivita na Uhalifu dhidi ya Binadamu na aina zote za Ubaguzi;

d) Itifaki ya Mkutano wa Kimataifa wa Maziwa Makuu ya Kuzuia na Kukomesha Ukatili wa Kingono dhidi ya Wanawake na Watoto;

e) Mkataba wa Kimataifa wa Kuwalinda Watu Wote Dhidi ya Kupotezwa, Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika;

f) Mkataba Uliofanyiwa Marekebisho wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi, Itifaki A/P.1/12/99 Inayohusu Utaratibu wa Kuzuia Migogoro, Kudhibiti, Kutatua, Kudumisha Amani na Usalama (Itifaki ya Lomé);

g) Mkataba wa Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

h) Mkataba wa Kuanzisha Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Kusini;

i) Mkataba Uliounganishwa wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika; na

j) Mkataba Uliorekebishwa wa Umoja wa Kiuchumi na Kifedha wa Afrika Magharibi (Traité Modifié de l'Union Economique et Monétaire Ouest Africaine).

57. Kuhusiana na mauaji ya kimbari, bila shaka mojawapo ya aina mbaya zaidi ya ukiukaji wa haki za binadamu na za watu, Kifungu cha I cha Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari (Mkataba wa Mauaji ya Kimbari), ambao angalau Nchi thelathini na tano (35) za Afrika kwa sasa ni wanachama, kinaweka wajibu dhahiri kwa Nchi wanachama "kuzuia na

kuadhibu" mauaji ya kimbari. Kifungu hiki, hasa wajibu uliomo ndani yake wa kuadhibu, kinapaswa kusomwa pamoja na Kifungu cha VI cha Mkataba, ambacho kinahitaji kwamba wahusika wa mauaji ya kimbari "watahukumiwa na mahakama yenye uwezo ya Nchi katika eneo ambapo kitendo hicho kilifanywa au na mahakama ya kimataifa ya makosa ya jinai ambayo inaweza kuwa na mamlaka kuhusiana na Wahusika wa Mkataba ambao watakuwa wamekubali mamlaka yake."

58. Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) mara kadhaa [tazama Kesi Kuhusu Matumizi ya Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari (Bosnia na Herzegovina dhidi ya Serbia na Montenegro),[63] na Kesi Kuhusu Matumizi ya Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari (Bosnia na Herzegovina dhidi ya Yugoslavia)][64] imethibitisha hali ya lazima ya wajibu wa kuadhibu mauaji ya kimbari kwa mujibu wa Mkataba na maslahi ya pamoja ya Nchi zote Wanachama katika kuhakikisha adhabu/mashtaka yanafunguliwa. Kwa umahususi, hivi karibuni katika Matumizi ya Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari (Gambia dhidi ya Myanmar),[65] Mahakama ya Kimataifa ya Haki iliamua kwamba Nchi Wanachama zote si tu kwamba zina maslahi ya pamoja katika kutoa adhabu ya mauaji ya kimbari na hivyo zimejizatiti kutimiza wajibu huu, bali kwamba wajibu huo pia ni wa asili ya erga omnes partes, kwa kuwa kila Nchi Mwanachama ina maslahi katika kuufuata na hivyo ina haki ya kuiwajibisha Nchi nyingine Mwanachama kwa kushindwa kutimiza wajibu huo.

59. Aidha, katika Kesi Inayohusu Shughuli za Kijeshi katika Eneo la Kongo (Maombi Mapya: 2002) (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo dhidi ya

---

[63]Kesi Inayohusu Utekelezaji wa Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari (Bosnia na Herzegovina dhidi ya Serbia na Montenegro), Mahakama ya Kimataifa ya Haki, Hukumu, tarehe 26 Februari 2007, I.C.J. Reports 2007, uk. 43 [162].

[64]Mahakama ya Kimataifa ya Haki, Hukumu, Mapingamizi ya Awali, tarehe 11 Julai 1996, Ripoti za I.C.J. 1996, uk. 595 [31–32].

[65]Mahakama ya Kimataifa ya Haki, Hukumu, Mapingamizi ya Awali, tarehe 22 Julai 2022, Ripoti za I.C.J. 2022, uk. 477 [107–109].

Rwanda), ICJ ilithibitisha marufuku dhidi ya mauaji ya kimbari kama kanuni ya jus cogens ambayo kwa hivyo inazifunga nchi zote bila kujali endapo ni wahusika wa Mkataba wa Mauaji ya Kimbari,[66] pia ilitoa maoni katika Reservations to the Convention on the Prevention and Punishment of the Crime of Genocide, Advisory Opinion[67] kwamba kanuni za Mkataba wa Mauaji ya Kimbari, ikiwemo wajibu wa kuadhibu mauaji ya kimbari, ni wajibu wa sheria ya kimkataba (Mkataba wa Mauaji ya Kimbari) na pia "unayafunga Mataifa, hata bila wajibu wowote wa kimkataba", kwa mujibu wa hadhi yake ya jus cogens. Kwa maneno mengine, wajibu wa kuadhibu mauaji ya kimbari ni wa lazima kwa Nchi zote bila kujali iwapo ni wanachama wa Mkataba wa Mauaji ya Kimbari.

60. Vifungu vya 8, 9, 10, 11 na 11 vya Itifaki ya Mkutano wa Kimataifa wa Maziwa Makuu ya Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari, Uhalifu wa kivita na Uhalifu dhidi ya Binadamu na Aina zote za Ubaguzi, 2006 pia vinatoa wajibu kwa Nchi Wanachama kuzuia na kuadhibu mauaji ya kimbari, uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu, huku Vifungu vya 2(2) na 4 vya Itifaki ya Mkutano wa Kimataifa wa Maziwa Makuu ya Kuzuia na Kukomesha Unyanyasaji wa Kingono dhidi ya Wanawake na Watoto, 2006 vikitoa wajibu kwa Nchi Wanachama kuadhibu unyanyasaji wa kingono ikiwemo kuhusiana na uhalifu wa mauaji ya kimbari, uhalifu dhidi ya binadamu na uhalifu wa kivita. Hadi sasa, vifungu hivi ndio uwekaji wa sheria ulio wazi zaidi na usio na utata barani Afrika kuhusu wajibu wa kufungua mashtaka dhidi ya baadhi ya hali zinazodhihirika zaidi za ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya sana wa haki za binadamu na watu, ambao ni mauaji ya kimbari, uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu.

[66]Kesi Inayohusu Shughuli za Kijeshi katika Eneo la Kongo (Maombi Mapya: 2002) (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo dhidi ya Rwanda), Mahakama ya Kimataifa ya Haki, Mamlaka ya Kisheria na Ukubalifu, Hukumu, tarehe 3 Februari 2006, Ripoti za I.C.J. 2006, uk. 6 [64].
[67]Masharti ya Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari, Maoni ya Ushauri ya tarehe 28 Mei 1951, Ripoti za I.C.J. 1951, uk. 15, 23.

61. Kuhusiana na vitendo vya mateso, Vifungu vya 4, 5, 7 na 8 vya Mkataba wa Kupinga Mateso na Adhabu au Vitendo Vingine vya Kikatili, Visiavyo vya Kibinadamu au Vinavyodhalilisha (Mkataba wa Kupinga Mateso)[68] unatoa wajibu kwa Nchi Wanachama kufanya vitendo vyote vya mateso kuwa kosa la jinai, uvichunguze, uvifungulie mashtaka na kuviadhibu. Kuhusu wajibu wa kufungua mashtaka, Kifungu cha 7 kinaweka wajibu mbadala wa ama kuwashtaki watuhumiwa wa ndani au kuwasafirisha kwenda kwenye nchi nyingine kwa ajili ya kushtakiwa.[69] Ingawa hakionyeshi kwa uwazi wajibu wa kufungua mashtaka, Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika pia kinapiga marufuku mateso,[70] huku Kifungu cha 16 cha Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) kikitoa wajibu kwa Nchi Wanachama kuchukua hatua za kuwalinda watoto dhidi ya mateso.

62. Sheria za kimataifa zimeidhinisha wajibu huu kwa Serikali kuhusiana na vitendo vya mateso. Kwa mfano, katika kesi ya Taasisi ya Haki za Binadamu na Maendeleo barani Afrika na Finders Group Initiative kwa niaba ya TFA (mtoto) dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Kameruni,[71] Kamati ya Afrika ya Haki na Ustawi wa Mtoto (Kamati ya Afrika) iliamua kwamba kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka kumi mara kwa mara ulikuwa aina ya mateso, kitendo kisichokuwa cha kibinadamu au cha kudhalilisha kwa mujibu wa Kifungu cha 16 cha ACRWC na kwamba kushindwa kwa Serikali

---

[68]Mkataba wa Kupinga Mateso na Adhabu au Mwenendo Mwingine wa Kikatili, Usio wa Kibinadamu au Unaodhalilisha, tarehe 10 Desemba 1984, 1465 UNTS 85; angalia pia Mkataba wa Nchi za Amerika wa Kuzuia na Kuadhibu Mateso, tarehe 9 Desemba 1985, Mfululizo wa Mikataba ya OAS 67, vifungu vya 6 na 12; Rasimu ya Vifungu vya Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu dhidi ya Binadamu, A/74/10, Kikao cha 71 cha ILC (Aprili–Agosti 2019), vifungu vya 10 na 13.

[69]Wajibu kama huo unapatikana, kuhusiana na wahusika wa utekaji na upotezaji, katika Kifungu cha 11 cha Mkataba wa Kimataifa wa Ulinzi wa Watu Wote dhidi ya Kupotezwa.

[70]Tume ya Afrika imeitafsiri kifungu hiki kuwa kinatoa wajibu wa kuwashtaki watendaji wa vitendo vya mateso. Angalia (Kisiwa cha Robben) Miongozo na Hatua za Kuzuia na Kukomesha Mateso, Adhabu au Vitendo vya Kikatili, Visivyo vya Kibinadamu au Vinavyodhalilisha barani Afrika (ACHPR/Res.61(XXXII)02), aya ya 4, 5, 6, 8 na 16; Azimio la Kuzuia na Kukomesha Mateso na Adhabu au Vitendo Vingine vya Kikatili, Visivyo vya Kibinadamu au Vinavyodhalilisha (ACHPR/Res.105(XXXXI)07), aya ya 3; Azimio la Haki ya Urejeshaji kwa Waathiriwa wa Mateso (ACHPR/Res.303(LVI)2015), aya ya 4.

[71]Mawasiliano namba 006/Com/002/2015, Uamuzi Na. 001/2018, uliopitishwa katika Kikao cha Kawaida cha 31 kilichofanyika mwezi Mei 2018, aya ya 57 na 77.

kuchunguza na kungua mashtaka dhidi ya mateso haya ilikiuka wajibu wake chini ya Kifungu cha 1 cha ACRWC cha kutekeleza haki ya msingi ya kutoteswa kama ilivyobainishwa chini ya Kifungu cha 16 cha ACRWC.

63. Mahakama ya Kimataifa ya Haki katika Masuala Yanayohusiana na Wajibu wa Kufungua Mashtaka au Kumsafirisha Mtuhumiwa Kwenda Nchi Nyengine (Ubelgiji dhidi ya Senegal),[72] ililinganisha na wajibu ulio chini ya Mkataba wa Mauaji ya Kimbari na ikasisitiza tena kwamba wajibu huo kwa mujibu wa Mkataba wa Kuzuia Mateso ni ya aina ya erga omnes partes, si tu yanayotakiwa kutekelezwa kwa waathiriwa/wahanga, bali pia na kwa Nchi Wanachama dhidi ya nyingine.

64. Kwa kutafsiri Kifungu cha 3 cha Mkataba wa Ulinzi wa Haki za Binadamu na Uhuru wa Msingi (Mkataba wa Ulaya wa Haki za Binadamu), ambacho kinakataza mateso na vitendo au adhabu ya kinyama au ya kudhalilisha, Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu iliamua katika hukumu yake ya mwaka 2014 katika Kesi ya Al Nashiri dhidi ya Polandi,[73] kwamba Mataifa yanawajibka kwa waathiriwa/wahanga na kwa umma kwa ujumla wa kutoa suluhu kwa waathiriwa wa mateso, ambayo ni ukiukaji mkubwa wa haki za

[72]Maswali Yanayohusiana na Wajibu wa Kufungulia Mashtaka au Kumsafirisha Mtuhumiwa Kwenda Nchi Nyingine (Ubelgiji dhidi ya Senegali), Mahakama ya Kimataifa ya Haki, Hukumu, tarehe 20 Julai 2012, Ripoti za I.C.J. 2012, uk. 422 [68]. Kuhusu wajibu wa erga omnes kwa ujumla, ICJ ilithibitisha kama ifuatavyo katika Kesi Kuhusu Kampuni ya Barcelona Traction, Light and Power Company Limited (Maombi Mapya: 1962) (Ubelgiji dhidi ya Uhispania), Mahakama ya Kimataifa ya Haki, Awamu ya Pili, Hukumu, tarehe 5 Februari 1970, Ripoti za I.C.J. 1970, uk. 3 [33-34]: "33. […] Kwa umahususi, tofauti muhimu inapaswa kuwepo kati ya wajibu wa Serikali kwa jumuiya ya kimataifa kwa ujumla, na yale yanayotokana na Serikali nyingine katika uwanja wa ulinzi wa kidiplomasia. Kwa asili yake, ya kwanza ni jambo linaloyahusu Mataifa yote. Kwa kuzingatia umuhimu wa haki zinazohusika, Mataifa yote yanaweza kuchukuliwa kuwa na maslahi ya kisheria katika ulinzi wao: ni wajibu wa erga omnes. 34. Kwa mfano, wajibu huo unatokana na sheria ya kimataifa ya sasa, na kupigwa marufuku kwa vitendo vya uvamizi na mauaji ya kimbari, na pia kutokana na kanuni na sheria zinazohusu haki za msingi za binadamu, ikiwemo ulinzi dhidi ya utumwa na ubaguzi wa rangi. Baadhi ya haki zinazohusiana za ulinzi zimeingia katika sheria ya jumla ya kimataifa (Masharti kwenye Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari, Maoni ya Ushauri, Ripoti za I.C.J. 1951, uk. 23); nyingine zimetolewa na hati zingine za kimataifa zenye sifa ya ulimwngu wote au kikanda."

[73]Maombi Na. 28761/11, Hukumu, tarehe 24 Julai 2014, aya za 495–499. Angalia pia Kesi ya El-Masri dhidi ya Jamhuri ya zamani ya Yugoslavia ya Masedonia, Maombi Na. 39630/90, Hukumu, tarehe 13 Desemba 2012, aya ya 182–192; Kesi ya Al-Skeini na wengine dhidi ya Uingereza, Maombi Na. 55721/07, Hukumu, tarehe 7 Julai 2011, aya za 161–167; Kesi ya Anguelova dhidi ya Bulgaria, Maombi Na. 38361/97, Hukumu, tarehe 13 Juni 2002, aya za 136–140.

binadamu, na ambayo suluhu inapaswa kujumuisha uchunguzi wa haraka, wa kina na wenye ufanisi na "uwajibikaji sahihi."

65. Kutokana na mjadala hapo juu, ni dhahiri kwamba wajibu wa kufungua mashtaka dhidi ya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu, kwa namna yoyote unavyojitokeza au kufanywa na kwa jina lolote linalotumiwa, ni wajibu wa kimkataba (unaotokana na Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika na vifungu husika vya mikataba iliyotajwa) na wajibu wa sheria ya kimataifa ya kidesturi, hasa kwa ukiukaji wa kanuni za jus cogens kama vile mauaji ya kimbari[74] na mateso.

***C. Utekelezaji wa wajibu wa kuchunguza na kufungua mashtaka nje ya mipaka ya nchi***

66. PALU inawasilisha kwamba wajibu wa kuchunguza na kufungua mashtaka dhidi ya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika hauishii tu kwenye ukiukaji huo uliofanywa katika eneo la Nchi husika. Kwanza, PALU inawasilisha kwamba Nchi mwanachama wa Mkataba wa Afrika ina wajibu huu kwa raia wake popote walipo, ikiwemo wanapokuwa ndani ya eneo la Nchi nyingine. Pili, wajibu huu erga omnes kwanza ni wajibu wa jumuiya ya kimataifa, na hasa kwa Mataifa ya Afrika kupitia Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya Kikatiba, pamoja na kupitia utendaji thabiti wa serikali ndani ya Umoja wa Afrika. Tatu, heshima ipasayo inapaswa kutolewa kwa falsafa na maadili ya Kiafrika, ikiwemo kanuni za maendeleo ya pamoja na ya jumuiya kama vile Ubuntu, kama ushahidi wa opinio juris ya Kiafrika na kama msingi wa mbinu ya pamoja ya Kiafrika ya uingiliaji kati nje ya mipaka ya nchi. Hoja hizi kwa

[74]Angalia, kwa mfano, Kesi Inayohusu Shughuli za Kijeshi katika Eneo la Kongo (Maombi Mapya: 2002) (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo dhidi ya Rwanda), Mahakama ya Kimataifa ya Haki, Mamlaka na Ustahiki, Hukumu, tarehe 3 Februari 2006, Ripoti za I.C.J. 2006, uk. 6 [64]; Reservations to the Convention on the Prevention and Punishment of the Crime of Genocide, Maoni ya Ushauri ya tarehe 28 Mei 1951, I.C.J. Reports 1951, uk. 15, 23.

pamoja zinaunga mkono wajibu kwa Mataifa ya Afrika ambao unaenea kwa watu wengine Waafrika popote walipo.

67. Kwa hivyo wajibu wa kuchunguza na kufungua mashataka ni wa ndani ya nchi na nje ya mipaka ya nchi. Kwa hivyo, bila kujali ni wapi barani Afrika ukiukaji huu unafanyika, Serikali ambayo ni mhusika wa Mkataba wa Afrika ina wajibu wa kuwashtaki wahusika, huku wajibu huo ukitekelezwa na Serikali ama kwa kushughulikia mashtaka yenyewe au kwa kushirikiana na Serikali au chombo kingine chochote ambacho kina uwezo wa kufungua mashtaka.

**(i) Mamlaka ya haiba amilifu na si amilifu**

68. Ingawa Mkataba wa Afrika haubainishi waziwazi au kuweka kikomo kwenye mawanda yake ya kijiografia, busara za kisheria za mfumo wa haki za binadamu wa Afrika kuhusu hali ya wajibu wa Nchi wa kuvuka mipaka ya nchi kwa mujibu wa Mkataba huo ni dhahiri kiasi ambapo Nchi au raia wake ndio wahusika wa ukiukaji katika eneo la Nchi nyingine ya Afrika (mamlaka ya haiba amilifu na si amilifu). Kwa mfano, katika hukumu yake ya mwaka 2022 katika kesi ya Bernard Anbataayela Mornah dhidi ya Jamhuri ya Benin na Wengine 7, Mahakama ya Afrika ilibainisha kuongezeka kwa utambuzi katika busara ya kimahakama ya kimataifa ya haki za binadamu kuhusu matumizi ya nje ya mipaka ya nchi kwenye mikataba ya haki za binadamu, hasa "kwenye maeneo ambayo Mataifa yana udhibiti madhubuti na kwa vitendo na kutotenda kunakofanywa na mawakala wao au watu walio chini ya ushawishi wao wa kijeshi, kisiasa na kiuchumi."[75] Ilisema kwamba "kuna kuongezeka kwa makubaliano kwamba wajibu wa kulinda au angalau, kutokiuka haki za binadamu unaenda zaidi ya mipaka ya jadi ya Nchi."[76]

---

[75]Supra, fn 31 hapo juu, aya ya 148.
[76]Maombi Na. 028/2018, Hukumu, tarehe 22 Septemba 2022, fungu la 149. Angalia pia Matokeo ya Kisheria ya Ujenzi wa Ukuta katika Eneo la Palestina Linalokaliwa na Wengine, Mahakama ya Kimataifa ya Haki, Maoni ya Ushauri, tarehe 9 Julai 2004, Ripoti za I.C.J. 2004, uk. 136 [107–112]; Kesi Kuhusu Shughuli za Silaha katika Eneo la Kongo (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo dhidi ya Uganda), Mahakama ya Kimataifa ya Haki, Hukumu, tarehe 19 Desemba 2005, Ripoti za

69. Tume ya Afrika iliweka msimamo kama huo hapo awali katika kesi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo dhidi ya Burundi, Rwanda na Uganda,[77] ambapo iliona kuwa Wasilisho lilkuwa na ukubalifu na ikaendelea kuona kuwa Burundi, Rwanda na Uganda zinawajibika kwa ukiukaji mkubwa na wa hali ya juu wa haki za binadamu na watu uliofanywa na wanajeshi wao katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hivi karibuni katika kesi ya Mohammed Abdullah Saleh al-Asad dhidi ya Jamhuri ya Djibouti,[78] Tume ilisisitiza zaidi, ikisema kwamba Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika "hakizuii waziwazi matumizi ya Mkataba ndani ya eneo na mamlaka ya Nchi Wanachama," na kwamba "mazingira yanaweza kutokea ambapo serikali inachukua majukumu zaidi ya mamlaka yake ya kieneo kama vile wakati ambapo serikali inachukua udhibiti halisi wa sehemu ya eneo la serikali nyingine (mfumo wa kieneo wa mamlaka), au ambapo serikali inatumia udhibiti au mamlaka kwa mtu binafsi (mfumo wa mamlaka kwa mtu binafsi)."

70. Sheria isiyo ya lazima ya Tume ya Afrika pia inathibitisha msimamo huu, ikiwemo Maoni ya Jumla Na. 3 kuhusu Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki ya Kuishi (Kifungu cha 4), ambapo Tume inasema, kwa kurejelea hasa haki ya kuishi, kwamba wajibu wa Serikali katika suala hili unahusu watu walio nje ya eneo lake ambapo "Serikali ina mamlaka ya kisheria au vinginevyo inatumia mamlaka, uwezo au udhibiti halisi kwa mhalifu au mwathiriwa (au haki za mwathiriwa), au inadhibiti kwa ufanisi eneo ambalo haki za mwathiriwa zinaathiriwa, au ikiwa Serikali inajihusisha na mwenendo ambao unaweza kutabiriwa kwa busara kwamba utasababisha kunyimwa uhai kinyume cha sheria,"[79] aidha, "Nchi za Nyumbani pia zinapaswa kuhakikisha uwajibikaji kwa ukiukaji wowote

I.C.J. 2005, uk. 168 [178–180]; angalia pia Suala la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo dhidi ya Jamhuri ya Rwanda, Hukumu (Mamlaka ya Kisheria na Ukubalifu), tarehe 26 Juni 2025, AFCHPR App. Na. 007/2023.

[77]Mawasiliano namba 227/99, yaliyopitishwa katika Kikao cha Kawaida cha 33 kilichofanyika tarehe 19–29 Mei 2003 – imefikiwa tarehe 22 Agosti 2025.

[78]Mawasiliano namba 383/10, yaliyopitishwa katika Kikao cha Kawaida cha 55 kilichofanyika kuanzia tarehe 28 Aprili 2014–12 Mei 2014, aya ya 134 – imefikiwa tarehe 22 Agosti 2025.

[79]Yamepitishwa katika Kikao cha Kawaida cha 57 kilichofanyika kuanzia tarehe 04–18 Novemba 2015, aya ya 14.

wa haki ya kuishi nje ya eneo lake, ikiwemo ule unaofanywa au kuchangiwa na raia wao au na biashara zilizo katika eneo au mamlaka yao."[80]

71. Vivyo hivyo, wajibu wa Mkataba wa Afrika unatimizwa na Nchi kwa raia wake, popote walipo barani Afrika. Kwa hivyo, wajibu wa kufungua mashtaka dhidi ya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na za watu kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika pia unatumika nje ya nchi ambapo raia wa Nchi ni mwathiriwa/mhanga wa ukiukaji uliofanywa nje ya eneo la Nchi hiyo (haiba si amilifu ya mamlaka).

**(ii) Wajibu wa mamlaka ya kimataifa**

72. Pale ambapo ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu haukufanywa kwenye eneo la Serikali (au eneo linalodhibiti) wala na au dhidi ya raia wake, busara ya kisheria ya mfumo wa haki za binadamu wa Afrika kuhusu wajibu wa nje ya eneo la Serikali hiyo haiko wazi sana. Kwa kawaida, mataifa hutumia mamlaka ya kisheria ndani ya maeneo yao wenyewe. Hata hivyo, katika mazingira mahususi, sheria ya kimataifa inawaruhusu kutunga sheria au kufungua mashtaka dhidi ya uhalifu uliofanywa nje ya mipaka yao na ambao hauna uhusiano wa moja kwa moja na wao. PALU inawasilisha kwamba sheria ya kimataifa inaweza kuwawezesha, au kuwawajibisha, Mataifa kuhakikisha uwajibikaji wa jinai unafanywa kwa ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu bila kujali mahali ambapo uhalifu huo ulitokea au utaifa wa waathiriwa/wahanga au wahalifu. Uzito wa makosa haya, ambao ni ukiukaji wa wajibu wa erga omnes na ukiukaji wa kanuni za jus cogens,[81]

[80] Yalipitishwa katika Kikao cha Kawaida cha 57 kilichofanyika tarehe 4–18 Novemba 2015, aya ya 18.

[81] Katika Kesi Kuhusu Kampuni ya Barcelona Traction, Light and Power Company Limited (Maombi Mapya: 1962) (Ubelgiji dhidi ya Uhispania), Mahakama ya Kimataifa ya Haki, Awamu ya Pili, Hukumu, tarehe 5 Februari 1970, Ripoti za I.C.J. 1970, uk. 3 [33–34], ICJ ilifafanua wajibu wa erga omnes kuwa 'wajibu wa Serikali kwa jumuiya ya kimataifa kwa ujumla … [ambayo] [kwa asili yake … ni ya nchi zote [na] kutokana na umuhimu wa haki husika, Nchi zote zinaweza kuonekana kuwa na maslahi ya kisheria katika ulinzi wake … [na kwamba, wajibu huo, kwa mfano, unatokana na sheria ya kimataifa ya kisasa, kutokana na kupigwa marufuku kwa vitendo vya uvamizi na mauaji ya kimbari, vilevile kutokana na kanuni na sheria zinazohusu haki za msingi za binadamu, ikiwemo ulinzi dhidi ya utumwa na ubaguzi wa rangi'.

unahusisha wajibu wa kimataifa na wa pamoja wa kuhakikisha uwajibishaji wa jinai. Wajibu huu unatokana na vifungu vya wazi na vya kudikeza vya mikataba mbalimbali, pamoja na sheria ya kimataifa ya kidesturi.

73. Sheria na desturi inaonyesha hali ya kukubaliana inayoongezeka katika mfumo wa haki za binadamu wa Afrika kwamba, kama wajibu wa kufungua mashtaka dhidi ya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu ni wa asili ya erga omnes na mara nyingi unahusu ukiukaji wa kanuni za jus cogens, haujazuiliwa kwa eneo ambalo uhalifu unafanywa wala kwa mahitaji ya utaifa wa wahalifu au wahanga/waathiriwa. Katika hali hii, kiungo pekee kinachounganisha Nchi inayofungua mashtaka, Nchi husika, mhalifu na waathiriwa/wahanga ni kwamba Nchi zote mbili ni wahusika wa Mkataba wa Afrika, kwa hivyo wajibu ulio hapa unatokana na uhusiano kati ya Nchi hizi na kwa watu wa Nchi hizi. Hasa, ndani ya muktadha wenye mipaka ya kijiografia wa bara la Afrika ambapo Mkataba wa Afrika unatumika, mkataba huo umepata kuridhiwa karibu na nchi zote, nchi 54 kati ya 55 za Afrika.

74. Ili kuelewa vizuri na kwa ukamilifu kiwango cha wajibu kwa mujibu wa Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika, kanuni ya mamlaka ya kimataifa lazima izingatiwe. Kwa mujibu wa kanuni hii, Mataifa yana wajibu wa kuingilia kati kupitia mashtaka katika hali za ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu hata pale ambapo ukiukaji huu haufanyiki kwenye maeneo yao (au maeneo wanayodhibiti) wala na au dhidi ya raia wao.

75. Kutambua kwa mara ya kwanza mamlaka ya kimataifa kwa mujibu wa sheria ya kimataifa ya kidesturi ulitokea katika muktadha wa uharamia, kanuni ambayo baadaye iliwekwa katika Kifungu cha 19 cha Mkataba wa Geneva wa mwaka 1958 kuhusu Bahari Kuu na Kifungu cha 105 cha Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1982 kuhusu Sheria ya Bahari,[82]

[82]Mkataba wa Geneva kuhusu Bahari Kuu (1958), kifungu cha 19; Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Sheria ya Bahari (1982), kifungu cha 105.

ukielezea kosa la uharamia kuwa kosa linalodhibitiwa na mamlaka ya kimataifa. Vivyo hivyo, Mikataba ya Geneva ya mwaka 1949 inahitaji waziwazi nchi wanachama kutumia mamlaka ya kimataifa kwenye ukiukaji mkubwa wa sheria ya kimataifa ya masuala ya kibinadamu.[83] Nchi wanachama zina wajibu wa kuwatafuta watu wanaodaiwa kufanya uhalifu huo, bila kujali utaifa wa mtuhumiwa, na kuwafikisha mbele ya mahakama zao za ndani au vinginevyo, kwa mujibu wa kanuni ya aut dedere aut judicare, kuwasafirisha kwenda nchi nyingine mwanachama ili wafikishwe mahakamani. Mikataba hii haihitaji uhusiano wowote wa eneo au uraia kati ya uhalifu na nchi inayofungua mashtaka.[84] Mfumo huu unaimarishwa zaidi na Itifaki ya Ziada ya I ya 1977 ya Mikataba ya Geneva, ambayo inapanua kanuni ya mamlaka ya kimataifa kwa ukiukaji mkubwa unaohusisha mwenendo wa uhasama katika mzozo wa kimataifa wa silaha, ikiainisha vitendo hivyo kuwa uhalifu wa kivita.[85]

76. Mkataba wa Kupinga Mateso pia unaweka mfumo wa lazima wa mamlaka ya kimataifa kwa kuhitaji Nchi Wanachama ziwe na mamlaka juu ya watuhumiwa wanaopatikana ndani ya eneo lao, bila kujali kosa hilo lilifanywa wapi au uraia wa wahusika.[86] Serikali lazima imshtaki mtuhumiwa au imkabidhi kwenye mamlaka ya kisheria iliyo tayari na inayoweza kumshitaki. Vivyo hivyo, Mkataba wa Kimataifa wa Kuwalinda Watu Wote Dhidi ya Kupotezwa unawajibisha nchi wanachama kuwa na mamlaka juu ya watuhumiwa waliopo katika eneo lao, bila kujali mahali uhalifu ulipotokea au utaifa wa mhalifu au mwathiriwa.[87] Kwa kurejelea kwa umahususi uhalifu wa mauaji ya kimbari, Mahakama ya Kimataifa ya Haki pia imekuwa na

[83]Mkataba wa Kwanza wa Geneva, kifungu cha 49; Mkataba wa Pili wa Geneva, kifungu cha 50; Mkataba wa Tatu wa Geneva, kifungu cha 129; Mkataba wa Nne wa Geneva, kifungu cha 146.
[84]Mikataba ya Geneva I–IV (1949), kifungu cha 49 cha GC I, 50 cha GC II, 129 cha GC III, 146 cha GC IV.
[85]Itifaki ya Ziada ya I (1977), kifungu cha 85. Angalia pia ICRC, Customary International Humanitarian Law, Juz. 1: Rules (Cambridge University Press 2005), kanuni ya 157.
[86]Mkataba wa Kupinga Mateso (1984), vifungu vya 5, 7. Angalia pia Mkataba wa Ljubljana-The Hague kuhusu Ushirikiano wa Kimataifa katika Uchunguzi na Kufungua Mashtaka dhidi ya Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari, Uhalifu dhidi ya Binadamu, Uhalifu wa Kivita na Uhalifu Mwingine wa Kimataifa (2023), kifungu cha 8(3).
[87]Mkataba wa Kimataifa wa Kuwalinda Watu Wote Dhidi ya Kupotezwa (2006), kifungu cha 9.

msimamo kwamba wajibu wa kuzuia na kuadhibu, kama ulivyowekwa katika Mkataba wa Mauaji ya Kimbari, una sifa ya erga omnes na kwa hivyo haujakomeshwa katika eneo ambalo uhalifu huo unafanywa [angalia Kesi Inayohusu Utekelezaji wa Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari (Bosnia na Herzegovina dhidi ya Yugoslavia)].[88] Kwa maneno mengine, wajibu wa kuadhibu uhalifu wa mauaji ya kimbari kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Mauaji ya Kimbari unatumika kwa Nchi Wanachama pale ambapo uhalifu huo unafanyika ndani ya eneo lao na nje ya eneo lao.

77. Mahususi kwa Afrika, PALU inasema kwamba mfumo wa kisheria na sera wa bara hili unatambua mamlaka ya kimataifa kama aina ya wajibu wa nje ya mipaka kwa Mataifa ya Afrika. Mapema mwaka 2006, Kamati ya Majaji Mashuhuri wa Afrika ya Umoja wa Afrika kuhusu Kesi ya Hissène Habré iliona kwamba Senegali, ambayo nchi ya Hissène Habré, na Nchi nyingine zote za Afrika zilizo wanachama wa Mkataba wa Kupinga mateso, zilikuwa na wajibu chini ya sheria ya kimataifa (na mamlaka ya kisheria), hasa unaotokana na Mkataba wa Kupinga Mateso, wa kumshitaki Habré, licha ya ukiukaji huo kufanywa nchini Chad na dhidi ya raia wa Chad.[89]

78. Mfumo wa kisheria wa Umoja wa Afrika, hasa Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, unatambua kwamba taasisi ya Umoja wa Afrika ina haki ya kuingilia kati kwenye Nchi Mwanachama wakati uhalifu mkubwa kama vile uhalifu wa kivita, mauaji ya kimbari na uhalifu dhidi ya binadamu unatokea kwenye Nchi Mwanachama.[90] Hasa, Kifungu cha 4(j) cha Sheria ya Kikatiba pia kinatambua haki ya Nchi yoyote Mwanachama wa Umoja wa Afrika "kuomba Umoja wa Afrika uingilie kati ili kurejesha

[88] Mahakama ya Kimataifa ya Haki, Hukumu, Mapingamizi ya Awali, tarehe 11 Julai 1996, Ripoti za I.C.J. 1996, uk. 595 [31] – imefikiwa tarehe 22 Agosti 2025.
[89] Ripoti ya Kamati ya Majaji Mashuhuri wa Afrika kuhusu Kesi ya Hissène Habré (2006), aya za 16–21, 28–29 na 33. Hasa, Kifungu cha 7 cha Mkataba wa Kupinga Mateso kinabainisha wajibu wa kumshitaki au kumsafirisha mtu anayeshukiwa kufanya mateso kwenda nchi nyingine ili ashitakiwe.
[90] Angalia pia Kanuni za Pretoria za Kukomesha Ukatili wa Halaiki kwa mujibu wa Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, 2012.

amani na usalama". Hali ya tafasiri ya wazi ya kifungu hiki inamaanisha kwamba Nchi Mwanachama inaweza kuomba Umoja wa Afrika uingilie kati katika eneo lake au katika eneo la Nchi Mwanachama nyingine na kwa namna yoyote ile ikiwemo kupitia uwajibishaji wa jinai. Vifungu hivi, vikichukuliwa kwa pamoja, vinaashiria utambuzi wa Nchi za Afrika kwamba ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu unatishia sana amani na usalama wa bara zima na kwa hivyo Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika, kwa pamoja chini ya Umoja wa Afrika au kila moja kivyake, zina maslahi katika kuzuia au kushughulikia ukiukaji huu. Aidha, Vifungu vya 3(a) na 3(e) vya Sheria ya Kikatiba vinaonyesha mshikamano na ushirikiano wa kimataifa kama kanuni muhimu zinazoongoza Umoja wa Afrika. Hii pia inaonekana katika Kifungu cha 23 cha Mkataba wa Afrika, ambacho kinatoa wito kwa Nchi Wanachama kushirikiana ili kudumisha amani na usalama. PALU inawasilisha kwamba vifungu hivi vya sheria, vikiangaliwa kwa pamoja, vinaunda msingi wa mamlaka ya kimataifa ndani ya mfumo wa kisheria wa bara, vikionyesha muktadha wa kisheria, kisiasa na kihistoria wa bara hili.

79. Vifungu hivi vya kisheria vimeimarishwa na mfumo wa sera wa Umoja wa Afrika pamoja na sheria isiyo ya lazima. Mwaka 2012, Umoja wa Afrika ulipitisha Sheria ya Kitaifa ya Kielelezo kuhusu Mamlaka ya Kisheria ya Kimataifa kwenye Uhalifu wa Kimataifa ambayo, kulingana na malengo na kanuni za Umoja wa Afrika katika Kifungu cha 3(a), 3(e) na 4(h) cha Sheria ya Sheria ya Kikatiba, hutoa mfumo linganifu wa kisheria wa kuzipa mwongozo Nchi Wanachama katika kutumia mamlaka ya kisheria ya kimataifa kwa ufanisi katika nchi zao. Kwa kufanya hivyo, Umoja wa Afrika ulirejelea Mkataba wa Afrika, ukathibitisha tena kutambua kwake kwamba "uhalifu fulani unasababisha wasiwasi mkubwa zaidi kwa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika na jumuiya ya kimataifa kwa ujumla kiasi kwamba haupaswi kuachwa bila kuadhibiwa" na ukasisitiza umuhimu wa kuchukua

hatua za ndani ili kuhakikisha mashtaka yanafanywa kwa ufanisi.[91] Sheria ya Kielelezo inaweka kipaumbele kwenye kanuni ya ukamilishanaji kwa kusisitiza kwamba Serikali ambapo uhalifu wa kimataifa (ambao kulingana na fasili unajumuisha ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu) unaodaiwa kufanya ulitokea ina haki na wajibu wa msingi wa kuchunguza na kufungua mashtaka, kulingana na utayari na uwezo wake wa kufanya hivyo. Hata hivyo, pia inatambua kwamba mahakama za Nchi nyingine pia zitakuwa na mamlaka kwenye uhalifu huu ikiwa mtuhumiwa wa uhalifu yuko katika eneo lao. Vivyo hivyo, Sera ya Haki ya Mpito ya Umoja wa Afrika, 2019 inasisitiza uchunguzi na mashtaka kama sehemu muhimu za nguzo ya haki na uwajibikaji ya haki ya mpito na inasisitiza kuhusu mbinu kamili inayohusisha mwitikio wa ndani, ya mseto na ya kimataifa (kanda ndogo, kikanda na kimataifa) kama inavyofaa katika kuhakikisha mashtaka yanafunguliwa dhidi ya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu.[92]

80. Kutokana na yaliyotajwa hapo juu, ni dhahiri katika kuainisha wajibu wa Mataifa ya Afrika kuhusiana na wajibu binafsi wa jinai kwa watu wanaoshukiwa kufanya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu barani Afrika, na hasa vipengele vya nje ya mipaka vya wajibu huu, mamlaka ya kimataifa lazima yawe sehemu muhimu ya mjadala. Kwa maneno mengine, kutafuta haki na uwajibikaji kutokana na ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu barani Afrika hakuhusishi tu Mataifa ambayo ukiukaji ulitokea katika maeneo yake au uliotekelezwa na au dhidi ya raia wake, bali ni wajibu wa Mataifa yote ya Afrika kwa watu wote wa Afrika.

81. PALU inawasilisha kwamba Nchi Wanachama wa Mkataba wa Afrika zina wajibu wa kuwafungulia mashtaka wahusika wa ukiukaji mkubwa, wa hali

[91]Sheria ya Kitaifa ya Kielelezo kuhusu Mamlaka ya Kimataifa ya Mahakama kuhusu Uhalifu wa Kimataifa, 2012, utangulizi. Angalia pia Uamuzi kuhusu Sheria ya Kitaifa ya Muundo wa Umoja wa Afrika kuhusu Mamlaka ya Kimataifa kuhusu Uhalifu wa Kimataifa, Doc. EX.CL/731(XXI)c.
[92]Sera ya Haki ya Mpito ya Umoja wa Afrika (Februari 2019), aya za 77–82.

ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu bila kujali uhusiano wowote wa moja kwa moja na nchi yao au raia wao. Kwa umahususi zaidi, inawasilishwa kwamba:

a) Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika kinaweka wajibu kwa Mataifa ya Afrika kuchunguza na kufungua mashtaka dhidi ya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu.

b) Wajibu wa Nchi Mwanachama kwa mujibu wa aya (a) hapo juu hauishii katika eneo la Nchi pekee.

c) Mkataba wa Afrika unaweka wajibu wa ushirikiano na mshikamano kwa Mataifa ya Afrika; yaani, kushirikiana na nchi nyingine ili kuhakikisha haki zilizo kwenye Mkataba zinatambuliwa na kulindwa. Kwa hivyo, nchi wanachama wa Mkataba wa Afrika zina wajibu wa kuwashtaki wahusika wa ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu bila kujali uhusiano wowote wa moja kwa moja na nchi yao au uraia wao, maadamu ukiukaji huo umefanyika barani Afrika, uanachama wa mkataba huo ukiwa ni wa nchi za Afrika pekee. Kwa maneno mengine, kuna msingi wa kutosha unaotokana na Mkataba wa Afrika na sheria na utendaji wa mfumo wa haki za binadamu wa Afrika wa kudai kwamba Mkataba wa Afrika unaweka wajibu kwa Mataifa ya Afrika kutekeleza mamlaka nje ya mipaka ya nchi kwa mujibu wa kanuni za haiba amilifu, haiba si amilifu na mamlaka ya kimataifa ya kuwafungulia mashtaka wahusika wa ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na za watu barani Afrika.

***D. Wajibu husika wa pamoja wa nchi za Afrika chini ya uundaji wa Umoja wa Afrika***

82. PALU inawasilisha kwamba mbali na wajibu wa Mataifa ya Afrika kama Mataifa binafsi, Mataifa haya pia, kama jumuiya chini ya uundaji wa Umoja wa Afrika, ya wajibu husika unaotokana na Mkataba wa Afrika. Jambo kuu

katika wasilisho hili ni kwamba Umoja wa Afrika ni chombo cha pamoja cha Nchi za Afrika ambacho kupitia hicho nchi hizi zimekubali wajibu wa pamoja na ambacho kupitia hicho zinachukua hatua za pamoja.

83. Kwa mujibu wa Kifungu cha 3(h) cha Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika,[93] malengo ya Umoja wa Afrika yanajumuisha kukuza na kulinda haki za binadamu na watu kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na vyombo vingine husika vya haki za binadamu. Aidha, kwa mujibu wa Vifungu vya 4(m) na (o) vya Sheria ya Kikatiba, kanuni zinazoongoza utendaji wa Umoja wa Afrika ni pamoja na kuheshimu haki za binadamu na utawala wa sheria na kukataa kutowawajibisha wahalifu.

84. Kwa hivyo, Nchi za Afrika kama jumuiya chini ya mwavuli wa Umoja wa Afrika zimejizatiti kutetea na kulinda haki zote za binadamu na watu kama zilivyowekwa katika Mkataba wa Afrika na katika hati zingine za haki za binadamu. Kuhusu matokeo ya vifungu vilivyotajwa hapo juu, baadhi ya wachambuzi wametoa madai sahihi kwamba, "Mbali na wajibu binafsi wa nchi wanachama kuhakikisha uzingatiaji wa haki za binadamu ndani ya mamlaka zao, Umoja wa Afrika wenyewe umechukua wajibu wa kitaasisi wa kuhakikisha uzingatiaji wenye ufanisi wa haki za binadamu barani Afrika kwa ujumla."[94] Kwa hivyo Mkataba wa Afrika unatoa mwongozo wenye mamlaka kwa Umoja wa Afrika kama uwakilishi wa pamoja wa Nchi zote za Afrika kuhusu masuala yote yanayohusu haki za binadamu na watu.

85. Vifungu ambavyo vina umuhimu wa kipekee kwenye Ombi hili ni Vifungu vya 4(h)[95] na (j)[96] vya Sheria ya Kikatiba, ambavyo vinaweka katika kanuni

---

[93]Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, tarehe 11 Julai 2000, 2158 UNTS 3.
[94]Ademola Abass and Mashood A. Baderin, ‘Towards Effective Collective Security and Human Rights Protection in Africa: An Assessment of the Constitutive Act of the African Union’ XLIX Netherlands International Law Review 1, 29 (2002). Angalia pia Owiso Owiso, 'A Cosmopolitan International Law: The Authority of Regional Inter-Governmental Obligations to Establish International Criminal Accountability Mechanisms' (Tasnifu ya Udaktari, Chuo Kikuu cha Luxembourg 2022), sura ya 6.
[95]Angalia pia Kifungu cha 4(j) cha Itifaki Inayohusu Uundaji wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika.
[96]Masharti kama hayo pia yanapatikana katika Kifungu cha 8(2) cha Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Ulinzi na Usaidizi kwa Watu Waliohamishwa Makwao Barani Afrika, 2009, na katika Kifungu

haki ya kiutaratibu au mamlaka ya Nchi za Afrika kuingilia kati kwa pamoja kupitia Umoja wa Afrika, ili kuendeleza na kutekeleza wajibu wa msingi uliojadiliwa hapo juu.

86. Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya Kikatiba kinaweka katika sheria "haki ya Umoja wa Afrika kuingilia kati katika Nchi Wanachama kwa mujibu wa uamuzi wa Mkutano Mkuu kuhusiana na hali mbaya, yaani: uhalifu wa kivita, mauaji ya kimbari na uhalifu dhidi ya binadamu", ilhali Kifungu cha 4(j) kinaweka katika sheria "haki ya Nchi Wanachama kuomba Umoja wa Afrika uingilie kati ili kurejesha amani na usalama ndani ya eneo lake au ndani ya eneo la Nchi nyingine Mwanachama."[97]

87. Mleta Maombi anarejea uwasilishaji wake wa awali kwamba uhalifu wa kivita, mauaji ya kimbari na uhalifu dhidi ya binadamu, unaojulikana kama "hali mbaya" katika Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya Kikatiba, ni ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na za watu. Vivyo hivyo, ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu kwa asili unatishia amani na usalama wa kitaifa na wa bara, kwa hivyo

---

cha 4(k) cha Itifaki Inayohusiana na Kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika.

[97] Angalia Owiso Owiso, 'A Cosmopolitan International Law: The Authority of Regional Inter-Governmental Obligations to Establish International Criminal Accountability Mechanisms' (Tasnifu ya Udaktari, Chuo Kikuu cha Luxembourg 2022), 166–172; Dire Tladi na John Dugard, 'The African Union's Right to Intervene and the Right to Life: Tension or Concordance?' katika Frans Viljoen na wengine (wahariri), A Life Interrupted: Essays in Honour of the Lives and Legacies of Christof Heyns (Pretoria University Law Press 2022) 258–265; Busingye Kabumba, 'Soft Law and Legitimacy in the African Union: The Case of the Pretoria Principles on Ending Mass Atrocities Pursuant to Article 4(h) of the AU Constitutive Act' katika Ololade Shyllon (mhariri), The Model Law on Access to Information for Africa and other Regional Instruments: Soft Law and Human Rights in Africa (Pretoria University Law Press 2018) 179–187; Eki Yemisi Omorogbe, 'The African Union, Responsibility to Protect and the Libyan Crisis' 59 Netherlands International Law Review 141, 149–152 (2012); Ntombizozuko Dyani-Mhango, 'Reflections on the African Union's Right to Intervene' (2012) 38 Brooklyn Journal of International Law 1, 11–17; Abdulqawi A. Yusuf, 'The Right of Forcible Intervention in Certain Conflicts' katika Abdulqawi A. Yusuf na Fatsah Ouguergouz (wahariri), The African Union: Legal and Institutional Framework – A Manual on the Pan-African Organization (Martinus Nijhoff Publishers 2012) 339–342; Dan Kuwali, 'The End of Humanitarian Intervention: Evaluation of the African Union's Right of Intervention' (2009) 9 African Journal on Conflict Resolution 41, 44–50.

unaonekana kuwa ndio unaounda mada ya maombi ya kuingilia kati kwa mujibu wa Kifungu cha 4(j) cha Sheria ya Kikatiba.[98]

88. Utendaji wa Umoja wa Afrika unathibitisha kwamba Umoja wa Afrika unaona kuwa uwajibikaji dhidi ya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu uko ndani ya mamlaka yake. Kwa mfano, kufuatia pendekezo la mwaka 2006 la Kamati ya Majaji Mashuhuri wa Afrika ya Umoja wa Afrika kuhusu Kesi ya Hissène Habré,[99] mwaka 2007 Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, ukitaja Vifungu vya 3(h), 4(h) na 4(o) vya Sheria ya Kikatiba, ulithibitisha kwamba "uhalifu ambao kwa huo Hissène Habré anashtakiwa [mateso] uko ndani ya uwezo wa Umoja wa Afrika"[100] na uliamuru Senegali "kufungua mashtaka na kuhakikisha kwamba Hissène Habré anahukumiwa, kwa niaba ya Afrika, kupitia mahakama yenye uwezo ya Senegali kukiwa na hakikisho la kusikilizwa kwa haki."[101] Mwaka 2009, Jopo la Ngazi ya Juu la Umoja wa Afrika kuhusu Darfur lilipendekeza Mahakama Mseto (kwa ajili ya Darfur) ili kufungua mashtaka dhidi ya ukiukaji mkubwa/mbaya wa haki za binadamu na watu huko Darfur na liliona kwamba Umoja wa Afrika utateua wafanyakazi wasio raia wa Sudan (kama wafanyakazi wa kuendesha mashtaka, usajili na uchunguzi) na pia kutekeleza jukumu muhimu katika kupendekeza na uteuzi wa majaji wasio raia wa Sudan katika mahakama hiyo.[102]

89. Vivyo hivyo, kwa kutambua wajibu wao wa pamoja chini ya uangalizi wa Umoja wa Afrika kama ilivyojadiliwa hapa, Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika wa Wakuu wa Nchi na Serikali ulipitisha Itifaki ya Marekebisho ya Itifaki ya Mkataba wa Mahakama ya Afrika ya Haki na Haki za Binadamu

[98] Angalia pia Utafiti wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki ya Mpito na Haki za Binadamu na Watu barani Afrika (2019), aya ya 173.
[99] Ripoti ya Kamati ya Majaji Mashuhuri wa Afrika kuhusu Kesi ya Hissène Habré (2006), aya za 16–21, 28–29 na 33.
[100] Assembly/AU/Dec.127(VII), aya ya 3 na 5(i).
[101] Mkutano/AU/Desemba.127(VII), aya ya 5(ii).
[102] Ripoti ya Jopo la Ngazi ya Juu la Umoja wa Afrika kuhusu Darfur, PSC/AHG/2(CCVII) (Oktoba 2009), aya za 246–254 na 322–333.

(Itifaki ya Malabo) tarehe 27 Juni 2014, ambayo, miongoni mwa mambo mengine, inataka kuanzisha sehemu ya sheria ya jinai ya kimataifa ya Mahakama ya Afrika ya Haki na Haki za Binadamu na Watu yenye mamlaka ya kisheria juu ya uhalifu wa kimataifa ikiwemo mauaji ya kimbari, uhalifu dhidi ya binadamu, uhalifu wa kivita, ugaidi, mamluki na biashara haramu ya kusafirisha watu, dawa za kulevya na taka hatari, ambayo yote ni ukiukaji mkubwa au mbaya wa haki za binadamu na watu. Hivi karibuni, mwezi Aprili 2024, Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika alimteua Mjumbe Maalumu wa kwanza kabisa wa Kuzuia Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari na Ukatili Mwingine kwa Watu, akisisitiza Nchi za Afrika kutambua janga la ukatili wa kijamii na uhitaji wa kuweka mkazo zaidi wa kulizuia.

90. Kwa hivyo PALU inawasilisha kwamba, pamoja na Vifungu vya 4(h) na (j) vinavyoweka sheria ya haki ya Nchi za Afrika kupitia Umoja wa Afrika kuingilia kati, kifungu hiki lazima pia kisomwe kama kinachoweka wajibu kwa Nchi za Afrika kupitia Umoja wa Afrika kuingilia kati katika hali za ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu barani Afrika.[103] Hii ni kweli hasa ikiwa, kama inavyopaswa kuwa lazima, Vifungu vya 4(h) na (j) vinasomwa pamoja na:

a) wajibu wa mshikamano na ushirikiano wa nchi za Umoja wa Afrika kwa mujibu wa vifungu vya 3(a), (h) na (e) vya Sheria ya Kikatiba, ambavyo vinaeleza "mshikamano kati ya nchi za Afrika na watu wa Afrika," kukuza na kulinda haki za binadamu na watu zilizowekwa katika Mkataba wa Afrika, na "ushirikiano wa kimataifa, kwa kuzingatia ipasavyo Mkataba wa Umoja wa Mataifa na Azimio la Haki za Binadamu"; na

b) Kifungu cha 23(1) cha Mkataba wa Afrika, ambacho kinasema, miongoni mwa mambo mengine, kwamba, "kanuni za mshikamano na

[103] Angalia pia Owiso Owiso, 'A Cosmopolitan International Law: The Authority of Regional Inter-Governmental Obligations to Establish International Criminal Accountability Mechanisms' (Tasnifu ya Udaktari, Chuo Kikuu cha Luxembourg 2022), 169–170; Ademola Abass, 'Prosecuting International Crimes in Africa: Rationale, Prospects and Challenges' (2013) 24 European Journal of International Law 933, 938.

uhusiano wa kirafiki zilizothibitishwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa na kuthibitishwa tena na ule wa Shirika la Umoja wa Afrika zitaongoza uhusiano kati ya Mataifa."

91. Tafsiri hii ya Vifungu vya 4(h) na (j) inaimarishwa zaidi na ukweli kwamba Nchi za Afrika zimejizatiti kisheria kwa mujibu wa Vifungu vya 4(m) na (o) vya Sheria ya Kikatiba kuheshimu haki za binadamu na utawala wa sheria na kukataa hali ya kutowawajibisha wahalifu barani Afrika.

***E. Wajibu husika wa pamoja wa nchi za Afrika chini ya uundaji wa Jumuiya Mbalimbali za Kiuchumi za Kikanda***

92. Kwa mujibu wa Kifungu cha 3(l) cha Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, mojawapo ya malengo ya Umoja wa Afrika ni "kuratibu na kuoanisha sera kati ya Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda zilizopo na za baadaye ili kufikia malengo ya Umoja wa Afrika hatua kwa hatua." Kwa hivyo ni dhahiri kwamba Sheria ya Kikatiba inaziona Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (REC) kama sehemu muhimu ya muundo wa Jumuiya ya Afrika, jambo linalomaanisha kwamba zinafungwa na kanuni na malengo ya Umoja wa Afrika, ikiwemo kama ilivyoelezwa katika Vifungu vya 3(a), (e) na (h) na 4(m) na (o) vya Sheria ya Kikatiba. Kwa maneno mengine, kama sehemu ya muundo wa utawala wa Umoja wa Afrika, Nchi za Afrika zina majukumu sawa ya pamoja ya mshikamano, ushirikiano na kuendeleza na kulinda haki za binadamu na watu chini ya uundaji wa Jumuia ya Kiuchimi za Kikanda kama zilivyo chini ya uundaji wa Umoja wa Afrika.

93. Aidha, hati za kisheria mahususi kwa Jumuiya mbalimbali za Kiuchumi za Kikanda pia huweka wajbu fulani wa pamoja kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya hizi za Kiuchumi za Kikanda kuhusiana na haki za binadamu na watu zilizowekwa katika Mkataba wa Afrika. Kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 4(g) cha Mkataba Uliorekebishwa wa Jumuiya ya Kiuchumi ya

Nchi za Afrika Magharibi, 1993 (Mkataba Uliorekebishwa wa ECOWAS),[104] Nchi wanachama kwa pamoja zimejifunga kwenye kanuni ya msingi ya "kutambua, kutetea na kulinda haki za binadamu na watu kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu."[105] Kifungu cha 56(2) cha Mkataba wa ECOWAS Uliorekebishwa kinaweka wajibu zaidi kwa Nchi hizi kushirikiana katika kutimiza malengo ya Mkataba wa Afrika. Kwa hivyo, Nchi Wanachama wa ECOWAS zimejizatiti kwa pamoja kutetea, kulinda na kutekeleza haki zote za binadamu na watu kama zilivyoainishwa katika Mkataba wa Afrika, ikiwemo kupitia ushirikiano.

94. Inafahamika pia kwamba Kifungu cha 3(h) cha Itifaki ya A/P.1/12/99 (Itifaki ya Lomé) kinaipa nguvu Nchi Wanachama wa ECOWAS kwa pamoja, chini ya mwongozo wa ECOWAS, "kuunda na kutuma kikosi cha kiraia na cha kijeshi ili kudumisha au kurejesha amani ndani ya eneo dogo, wakati wowote hitaji linapotokea." Kifungu cha 25(d) cha mkataba huo kinaidhinisha uingiliaji kati "katika tukio la ukiukaji mkubwa na wa hali ya juu wa haki za binadamu na utawala wa sheria."

95. Katika suala hili, PALU inawasilisha kwamba, kwanza, mazingira ambapo ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya sana wa haki za binadamu na watu unafanywa ni tishio kwa amani na usalama. Pili, baada ya kujizatiti kushirikiana katika kulinda na kuhakikisha haki za Mkataba wa Afrika kwa mujibu wa Vifungu vya 4(g) na 56(2) vya Mkataba wa ECOWAS Uliorekebishwa, Nchi Wanachama wa ECOWAS chini ya mwavuli wa pamoja wa ECOWAS zina wajibu wa kuingilia kati katika Nchi Mwanachama ambapo ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu umefanyika au unafanyika. Tatu, njia ya kuingilia kati

[104]Mkataba wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (uliopitishwa tarehe 24 Julai 1993, ulianza kutumika tarehe 23 Agosti 1995) (1996) 35 ILM 660 (Mkataba wa ECOWAS Uliorekebishwa).
[105]Angalia pia Kifungu cha 2 cha Itifaki A/P.1/12/99 Kuhusu Utaratibu wa Kuzuia Migogoro, Kudhibiti, Kutatua, Kudumisha Amani na Usalama (Itifaki ya Lomé).

inaweza kuwa kwa njia ya hatua za kijeshi au zisizo za kijeshi, ikiwemo mifumo ya uwajibikaji wa jinai.[106]

96. Vivyo hivyo, Mkataba wa Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (Mkataba wa EAC)[107] unaweka wajibu husika kwa Nchi Wanachama kwa pamoja chini ya uundaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hasa, Kifungu cha 5(3)(f) cha Mkataba wa EAC kinaamuru utetezi wa amani, usalama na utulivu kama lengo la msingi la Jumuiya, wakati Kifungu cha 6(d) kinajumuisha "utawala bora ikiwa ni pamoja na kuzingatia kanuni za demokrasia, utawala wa sheria, uwajibikaji, uwazi, haki ya kijamii, fursa sawa, usawa wa kijinsia, pamoja na kutambua, kutetea na kulinda haki za binadamu na watu kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu" kama kanuni za msingi za Jumuiya.

97. Malengo na kanuni zilizo hapo juu zinaimarishwa na wajibu kwa mujibu wa Kifungu cha 7(2) cha Mkataba wa EAC kwa Nchi Washirika "kuzingatia kanuni za utawala bora, ikiwemo kufuata kanuni za demokrasia, utawala wa sheria, haki ya kijamii na udumishaji wa viwango vya haki za binadamu vinavyokubalika ulimwenguni." Inaonekana wazi kwamba, Mahakama ya Afrika Mashariki imetaja mara nyingi kwamba utawala wa sheria, uwajibikaji na kanuni za haki za binadamu katika Kifungu cha 6(d) na wajibu kwa mujibu wa Kifungu cha 7(2), ziko dhahiri, mahususi, hazina utata na zinazoweza kutekelezwa/kuwasilishwa mahakamani [angalia kesi ya James Katabazi na wengine 21 dhidi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Uganda,[108] Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Kenya dhidi ya Independent Medical Legal Unit,[109]

---

[106]Azimio la Pamoja la Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi, Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa kuhusu Hali ya Kisiasa ya Jamhuri ya Kiislamu ya Gambia (lilipitishwa tarehe 21 Januari 2017). Angalia pia aya ya 59, Mawasiliano ya Mwisho, Kikao cha 66 cha Kawaida cha Mamlaka ya Wakuu wa Nchi na Serikali (yalipitishwa tarehe 15 Desemba 2024).
[107]Ilipitishwa tarehe 30 Novemba 1999, na kuanza kutumika tarehe 7 Julai 2000 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2006 na 2007).
[108]Kesi ya Rufaa ya EACJ ya 1 ya mwaka 2007, Hukumu, tarehe 1 Novemba 2007, uk. 15–23.
[109]Rufaa ya EACJ Na. 1 ya 2011, Hukumu, tarehe 15 Machi 2012, uk. 9–13 – imefikiwa tarehe 25 Novemba 2025.

Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Rwanda dhidi ya Plaxeda Rugumba,[110] Democratic Party dhidi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na wengine 4[111] na Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Uganda dhidi ya Tom Kyahurwenda.[112]

98. Aidha, Kifungu cha 6(e) cha Mkataba wa Kuanzisha Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Kusini (Mkataba wa COMESA)[113] kinajumuisha kutambua, kutetea na kulinga haki za binadamu na watu kwa mujibu wa masharti ya Mkataba wa Afrika, kama kanuni ya msingi ya COMESA. Kifungu hiki kinaimarishwa na Vifungu vya 6(f), (g) na (i), ambavyo vinathibitisha uwajibikaji, utawala wa sheria na udumishaji wa amani na usalama kama kanuni za msingi za COMESA. Vivyo hivyo, kwa mujibu wa Kifungu cha 4(c) cha Mkataba Uliounganishwa wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (Mkataba wa SADC), "haki za binadamu, demokrasia na utawala wa sheria" ni kanuni za msingi zinazoongoza Jumuiya na Baraza la Kisheria la SADC ambalo halifanyi kazi tena ilidai katika kesi ya Mike Campbell (PVT) Ltd na Wengine 78 dhidi ya Jamhuri ya Zimbabwe kwamba kanuni hizi zimeelezwa wazi na zinaweza kutekelezwa/kuwasilishwa mahakamani,[114] na kwa kufanya hivyo ilirejelea kwa kina wajibu wa Serikali chini ya Mkataba wa Afrika.

99. Kifungu cha 3 cha Mkataba Uliorekebishwa wa Umoja wa Kiuchumi na Kifedha wa Afrika Magharibi (Traité Modifié de l'Union Economique et Monétaire Ouest Africaine) (Mkataba Uliorekebishwa wa UEMOA) pia kinabainisha kwamba Nchi Wanachama wa Umoja huo kwa pamoja zinajizatiti kuheshimu "haki za msingi zilizowekwa katika Azimio la

[110] Rufaa ya EACJ 1 ya 2012, Hukumu, tarehe 22 Juni 2012, aya za 23–27 – ilifikiwa tarehe 25 Novemba 2025.
[111] Rufaa ya EACJ Na. 1 ya mwaka 2014, Hukumu, tarehe 28 Julai 2015, aya za 49–75 – ilifikiwa tarehe 25 Novemba 2025.
[112] Kesi ya EACJ iliyotajwa Nambari 1 ya 2014, Hukumu ya Awali, tarehe 31 Julai 2015, aya za 62–69 – ilifikiwa tarehe 25 Novemba 2025.
[113] Ilipitishwa tarehe 5 Novemba 1993, ilianza kutumika tarehe 8 Desemba 1994 (iliyorekebishwa mwaka 2009) (1994) 33 ILM 1067.
[114] Kesi ya SADCT Na. 2/2007 [2008] SADCT 2, Hukumu, tarehe 28 Novemba 2008, uk. 24–25 – ilifikiwa tarehe 23 Novemba 2025.

Kimataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981."

100. Kutokana na yaliyotajwa hapo juu, ni dhahiri kwamba Nchi za Afrika kwa pamoja, chini ya usimamizi wa jumuiya mbalimbali za REC, zina wajibu wa kufuata masharti ya Mkataba wa Afrika si kwa sababu tu jumuiya hizi za REC ni sehemu muhimu ya muundo wa Umoja wa Afrika, jambo ambalo linamaanisha kwamba zina wajibu, kama ilivyoelezwa katika masharti yaliyotajwa hapo juu ya Sheria ya Kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika, wa kutetea na kulinda haki za binadamu na watu kama zilivyoainishwa katika Mkataba wa Afrika. Hati za kikatiba za Jumuiya mbalimbali za Kiuchumi za Kikanda (REC) zinazitaka Nchi hizi kwa pamoja, chini ya uundaji wa Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (REC), zitetee na kulinda haki za binadamu na watu kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Afrika. Kwa hivyo, PALU inawasilisha kwamba Mataifa ya Afrika kwa pamoja, chini ya uundaji wa Jumuiya mbalimbali za Kiuchumi za Kikanda, zina wajibu wa kuhakikisha haki za Mkataba wa Afrika, na wajibu unaotokana nazo, kwa mujibu wa Kifungu cha 1 cha mkataba huo, na hii inajumuisha wajibu wa kushtaki ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu.

### *F. Msimamo wa PALU kuhusu Maswali Yaliyoulizwa*

101. Kwa kuzingatia hoja zilizotolewa hapa, PALU inawasilisha kwamba usomaji wa kukusudia na wa kjenga wa Kifungu cha 1 na 58(1)-(2) vya Mkataba wa Afrika na vifungu vya hati za kisheria zinazotumika zilizotajwa unapaswa kusababisha hitimisho lifuatalo:

    i. Kirai "ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu" unapaswa kueleweka kuwa unarejelea ukiukaji wa haki za binadamu na watu ulio mbaya sana na/au unaofanywa kwa njia ya kimfumo au kwa kiwango kikubwa na unajumuisha ukiukaji ule ambao

ni sawa na uhalifu wa kimataifa kama vile uhalifu wa kivita, mauaji ya kimbari na uhalifu dhidi ya binadamu.

ii. Nchi za Afrika zina wajibu kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika na kwa mujibu wa viwango husika vya kisheria vya kimataifa vilivyorejelewa vya kuchunguza kwa uzito, kwa haraka na kwa ufanisi ukiukaji mkubwa, wa kiwango kikubwa au mbaya wa haki za binadamu na watu barani Afrika na kuwafungulia mashtaka wahusika, bila kujali Nchi/eneo ambapo ukiukaji huu unafanywa na bila kujali utaifa wa watu wanaohusika.

iii. Kushindwa kwa Mataifa ya Afrika kuchunguza ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu barani Afrika na kuwafungulia mashtaka wale waliohusika ni ukiukaji wa wajibu wao kwa mujibu wa sheria za kimataifa.

iv. Nchi za Afrika kwa pamoja, chini ya mwamvuli wa Umoja wa Afrika na/au REC, kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika na viwango husika vya kisheria vya kimataifa vilivyorejelea, zina wajibu wa kuingilia kati iwapo kutatokea ukiukaji mkubwa, wa kiwango kikubwa au mbaya wa haki za binadamu na watu barani Afrika na kuchunguza ukiukaji huu na kusababisha wanaowajibika washtakiwe.

v. Mataifa ya Afrika kwa pamoja, chini ya mwamvuli wa Umoja wa Afrika na/au Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, kushindwa kuingilia kati, kuchunguza na kusababisha ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu barani Afrika kufunguliwa mashtaka kwa ufanisi ni ukiukaji wa wajibu wao wa pamoja kwa mujibu wa sheria ya kimataifa.

vi. Nchi za Afrika kwa pamoja, chini ya usimamizi wa Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika na viwango husika vya kisheria vya kimataifa vilivyorejelewa, zina wajibu wa jumla wa kushirikiana baina yao na pamoja na Umoja wa Afrika katika kuhakikisha uchunguzi makini, wa haraka na wenye ufanisi na kufungua mashataka

dhidi ya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu barani Afrika.

vii. Mataifa ya Afrika kwa pamoja, chini ya mwavuli wa Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, kushindwa kushirikiana na Umoja wa Afrika na wao kwa wao katika kuhakikisha uchunguzi makini, wa haraka na wenye ufanisi wa ukiukaji mkubwa au mbaya wa haki za binadamu na watu barani Afrika ni ukiukaji wa wajibu wa kwa mujibu wa sheria ya kimataifa.

102. Hitimisho katika aya ya 101 hapo juu linatokana na usomaji wa wazi na wa makusudi tafsiri ya vifungu vya mkataba vilivyorejelewa hapo juu na sheria ya kimataifa ya kidesturi, pamoja na busara ya kisheria yenye mamlaka na ya kushawishi ya mahakama za kimataifa, ikiwemo Mahakama hii Tukufu na mahakama nyingine za kimataifa, za kikanda na za kanda ndogo.

## VIII. MUHTASARI WA OMBI

103. Chama cha Wanasheria wa Afrika (PALU), shirika la Afrika linalotambuliwa na Umoja wa Afrika (AU), kimewasilisha Ombi la Maoni ya Ushauri mbele ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama).

104. PALU inatoa Ombi hili baada ya kushirikiana na mashirika ya kiraia ya Afrika, ikiwemo Atrocities Watch Africa, na wataalamu wengine wa kujitegemea kuhusu mifumo ya amani na usalama ya Umoja wa Afrika, Sheria ya Kimataifa ya Haki za Binadamu na Sheria ya Kimataifa ya Jinai.

105. Ombi hili linafanywa kwa mujibu wa Kifungu cha 4(1) cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu ya Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kikisomwa pamoja na Kanuni ya 82(1) ya Kanuni za Mahakama ya Afrika. PALU inasisitiza kwamba Mahakama hii ina mamlaka ya kisheria yanayohitajika ili kushughulikia Ombi hili, ambalo linahusu wajibu wa haki za binadamu wa Nchi za Afrika katika muktadha wa ukiukaji mkubwa na mbaya wa haki za binadamu.

106. Sheria ya msingi ambayo Ombi hili limejikita ni Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu. Ombi hili linalenga kupata tafsiri ya Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika kuhusiana na wajibu wa Mataifa ya Afrika, kila moja kivyake na kwa pamoja. PALU pia inarejelea inarejelea hati zingine za bara na kikanda, zikiwemo Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika (AU), Itifaki ya Lomé, Itifaki ya Mkutano wa Kimataifa wa Maziwa Makuu kuhusu Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari, Uhalifu wa Kivita na Uhalifu dhidi ya Binadamu na aina zote za Ubaguzi, Itifaki ya Mkutano wa Kimataifa wa Maziwa Makuu kuhusu Kuzuia na Kukomesha Unyanyasaji wa Kingono dhidi ya Wanawake na Watoto, Mkataba Uliorekebishwa wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi, Mkataba Uliorekebishwa wa Umoja wa Kiuchumi na Fedha wa Afrika Magharibi, Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mkataba Uliojumuishwa wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, na Mkataba wa Kuanzisha Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Kusini, kama miongozo ya tafsiri kwa Mahakama kuhusiana na kuamua wajibu wa Serikali kwa haki za watu binafsi na Watu, kama inavyohakikishwa chini ya Mkataba.

107. Ombi hili linatafuta ufafanuzi kuhusu iwapo, kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika ukisomwa peke yake au kwa pamoja na Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika na hati zingine husika, Nchi za Afrika zina wajibu wa kisheria wa kuzuia ukiukaji mkubwa na wa hali ya juu wa haki za binadamu na, pale ambapo ukiukaji huo unatokea, kuhakikisha wale wanaohusika wanawajibishwa kwa ufanisi. Aidha linauluza endapo wajibu wa Nchi kwa mujibu wa Kifungu cha 1 cha Mkataba kutumia hatua za kisheria na nyinginezo zikichukua hatua kivyake na kwa kushirikiana na Nchi nyingine, kunajumuisha wajibu wa kuhakikisha uwajibikaji wa makosa ya jinai ya mtu binafsi kwa ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu na watu.

108. Aidha, Ombi hili linatoa wito kwa Mahakama ifafanue kiwango ambacho Nchi za Afrika zinahitajika ili kuanzisha na kutekeleza mifumo madhubuti ya ushirikiano wa kikanda na bara, kupitia Umoja wa Afrika, Jumuiya za

Kiuchumi za Kikanda, au mifumo mingine, ili kuhakikisha uwajibikaji kwa uhalifu wa kimataifa unafanyika. Hatimaye, endapo wajibu wa aina hii kama ilivyodaiwa upo, ombi hili linatafuta mwongozo kuhusu matokeo ya kisheria yanayotokana na kukataa au kushindwa kwa Mataifa ya Afrika, yakitenda kivyake au kwa pamoja, kumkabidhi mtu kwa nchi nyingine au kumshitaki mtu anayeshukiwa kuwa ametenda uhalifu mkubwa wa kimataifa.

109. PALU inawasilisha kwamba Mataifa ya Afrika yana wajibu mara nne kwa mujibu wa sheria ya kimataifa ya haki za binadamu: kuheshimu, kulinda, kutetea na kutekeleza haki zilizohakikishwa, ikiwa ni pamoja na wajibu wa kuchukua hatua za kuhakikisha ulinzi wa haki hizi na wajibu unaotokana nazo kumwajibisha mtu kwa jinai yake katika ngazi ya bara, ya kikanda na ngazi nyinginezo, ikiwa ni pamoja na kitaifa.

110. Aidha, PALU inawasilisha kwamba kutangazwa na kutimizwa kwa wajibu uliopo wa aina hii, kama inavyodaiwa, ni muhimu kwa utekelezaji wa pamoja wa malengo ya maendeleo ya bara hili, ikiwemo masuala ya amani, usalama na haki ya mpito. Aidha, kutokuwajibika kwa wahalifu ni kinyume cha kupiga hatua na pengo lililopo la upatikanaji haki, kutokana na kutofafafanua vizuri wajibu wa nchi kuhusu suala hili, hali ambayo huzidisha zaidi uendelezaji wa ukatili wa halaiki dhidi ya watu wa Afrika.

## IX. HITIMISHO

111. Kutokana na yaliyotajwa hapo juu, PALU inawasilisha kwamba Ombi hili la Kupata Ushauri wa Kisheria linatoa fursa kwa Mahakama kubainisha, kufafanua na kuelezea kwa mamlaka wajibu wa Nchi za Afrika, nchi moja moja na kwa pamoja, chini ya miundo ya Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda za Afrika, kuhusiana na watu wanaotuhumiwa kufanya ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu barani Afrika.

112. Aidha, Mahakama inapewa fursa ya kukazia msimamo wake kama "jukwaa la bara zima kwa ajili ya majadiliano ya kanuni na desturi za haki za binadamu zinazotumika kwa nchi za Afrika … [na] kuainisha, kuhalalisha na kuendeleza vipaumbele vya haki za binadamu vya bara hili,"[115] hasa kuhusiana na uwajibikaji wa makosa ya jinai kwa mtu binafsi kutokana na ukiukaji mkubwa, wa hali ya juu au mbaya wa haki za binadamu na watu barani Afrika.

Imetiwa saini na kuwekwa tarehe jijini ARUSHA, JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA tarehe 24 Aprili 2025

______________________________

**MWANDISHI/MWAKILISHI**

Kwa ajili ya kuwasilishwa kwa:

Msajili wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

Kituo cha Uhifadhi cha Mwalimu Julius Nyerere

[115] Chidi Anselm Odinkalu, 'Advice without Consent?: Assessing the Advisory Jurisdiction of the African Court on Human and Peoples' Rights' (2023) 45(3) Human Rights Quarterly (Jarida la Haki za Binadamu) 365, 402–403.

Barabara ya Dodoma, S.L.P. 6274, Arusha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Barua pepe: registry@african-court.org

## FAHARISI YA VIAMBATISHO

1. Hati ya Makubaliano kati ya Chama cha Wanasheria wa Afrika na Umoja wa Afrika (2026)